




## Mwanafunzi wa darasa la nne akutwa akiwa amejinyonga

UKURASA 3


Chama chaazimia 'mama kwanza', ni juhudi kuondoa ubaguzi kisiasa

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

'BAI' MUHAMMADU BUHARI

Ni Nigeria na jambo lao, wagombea mvinyo wa zamani kwenye chupa mpya

Mwenyekiti AAFP aja na mkakati mikutano ya hadhara

■ Ni mkulima anayepinga chakula kuuzwa nje

UKURASA 11

Nipashe

Jumatano Februari 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581229


www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Wataka sheria kuwabana wanaume wasiolea watoto

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Mtukufu Sheikh Shakhboot Bin Nahyan aliyeambatana na ujumbe wake, Ikulu Tunguu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 3

## Watu saba wajeruhiwa na fisi wakienda shambani



Mmoja kati ya watu saba waliojeruhiwa na fisi, Francis Siongo akiwa amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara jana. **PICHA: SAMSON CHACHA**

## Samia, Hichilema wakubaliana kuboresha bomba la TAZAMA

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA: SASA NI ZAMU YA KMC** UK.24

**MAONI** UK.6




Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Kijiji cha Tongwe, wilayani Muheza mkoani Tanga, Charles Mahimbo (katikati), akiongoza ibada ya mazishi ya Christina Ngusi (23) katika kitongoji cha Masiwa jana. Ngusi anadaiwa kuuawa baada ya kuchomwa visu mwilini na mpenzi wake, Daktari Richard Bonifasi (28) katika eneo la Hospitali ya Teule Muheza Mjini. Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Erasto Mhina. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wataka sheria kuwabana wanaume wasiolea watoto

**Na Christina Mwakangale**

KASI ya ongezeko la malezi ya upande mmoja, hasa kinamama kulea peke yao, imewaibua wanaharakati, wakitaka sheria iliyopo kuongezewa makali ili kuwabana wakinababa wasiowajibika kwenye malezi.

Wanaharakati hao wameibuka huku Nipashe ikibaini kuwapo ongezeko kubwa la malezi ya upande mmoja yanayowahusisha wanawake (single mothers) ambayo yanatajwa kuchangia kuporomoka kwa maadili na ukatili dhidi ya watoto.

Sambamba na hao, wengine wenye umri kuanzia miaka mitatu na kuendelea wanaolelewa katika maeneo ya barabara kuu, yakiwamo makutano ya Mwenge, Buguruni, Ubungo darajani na eneo la Ubalozi, makutano ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Kinondoni.

Uchunguzi wa Nipashe katika masoko kadhaa ya Dar es Salaam, yakiwamo Mabibo, Kariakoo, Tegeta, Mbagala, Temeke na Buguruni, umeshuhudia wazazi wakiwa na watoto wao, baadhi wachanga wenye umri wa mwezi mmoja.

Udadisi wa Nipashe kwa mchuuzi wa bamia katika soko la Tegeta (jina tunalo), ili kupata undani wa hali hiyo, alipata ufafanuzi akisema: "Nimekuja na mtoto mchanga sokoni kutafuta riziki kwa sababu hakuna wa kunihudumia na mwenye mtoto alishaniacha tangu nikiwa na mimba."

"Unavyoniona hapa nimezalishwa watoto wawili, mwanamume kanitoroka kwenda kuishi na mwanamke mwingine. Ninalea wanangu mwenyewe, lazima nitokee nikahangaike kuwatafutia riziki kama hivi inabidi niuze nyanya," alisema mama mwingine.

Neema John anasema mke mwenzake alikimbiwa na mumewe akamwacha na watoto wadogo mmoja ana miezi sita na mkubwa miaka miwili, wakaishi naye kwenye vyumba viwili, hana kazi na wakati huo anatakiwa kulisha watoto.

Wadau na wanaharakati waliozungumza na mwandishi, walisema kuongezeka kwa hali hiyo nchini, kunatokana na sheria zilizopo kuwa butu na kwamba uwapo wa sheria kali itaongeza uwajibikaji wa pande zote; baba na mama.

Walisema sheria hiyo iweke wazi wazazi kupaswa kuwajibika na kuwabana wanaowatelekeza watoto na kwamba malezi hayo huchangia ukatili kwenye jamii.

Sheria Namba 21 ya Mtoto ya Mwaka 2009, inasema haki ya mtoto ni kulelewa na wazazi wote; baba na mama ili ikuimarisha ulinzi, matunzo na haki.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, akizungumza kuhusu suala hilo, alisema sheria bado ni butu pamoja na ustawi wa jamii kupewa jukumu la kusimamia hilo.

"Changamoto ni kubwa sana, 'single mothers, parents' kutokana na mifumo yetu ya kubana wanaopata watoto maana yake wa kike na kiume, ni dhaifu ustawi wa jamii ndio inawajibika lakini sheria za nchi bado hazijaweka uzatiti.

"Kwamba watu wawili wanapopata mtoto wote wanawajibika, ifike mahali tuwe na sheria kali, hata wawekwe ndani wale wanaotelekeza watoto, ndio maana ukatili wa watoto unaongezeka. Ili kupunguza lazima tupambane na mzazi mmoja kuachiwa mtoto," alisema.

"Utakuta wanaume wanakimbia wanakwenda kuanzisha familia huko kwingine, anamuacha mwanamke na watoto anahangaika kuwalea mwenyewe, akienda ustawi wa jamii hapati matuzo yanayostahili," alibainisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema pamoja na malezi ya watoto kwa kiwango kikubwa hivi sasa kuelemea upande wa wanawake, imebainika 'single mothers' wanamudu.

"Kwanza 'single mothers' wamethibitisha wanafanya vizuri kuliko 'single fathers'. Na ongezeko la watoto wa mtaani ni kutokana na kuvunjika kwa ndoa na namna ya kuishi maisha mapya baada ya ndoa kuvunjika, inasababisha waende kulelewa kwa shangazi au kuzagaa a," alisema Anna.

Alisema utafiti uliofanyika unaonyesha kwamba asilimia 50 ya watoto waliopo mitaani sababu kuu ni ndoa zilizovunjika na kusababisha malezi ya watoto kuwa duni.

"Sheria ya jinai na madai inatoa wajibu wa baba kulea familia yake, kulea watoto wake, kizazi chake, kuna sheria inalazimisha hivyo. Ingawa wanaotakiwa kufanya sheria itekelezeke wanakuwa walaini kidogo, lakini inatakiwa kufuatiliwa kwa kina," alisema Henga.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, alikemea tabia inayokithiri hivi sasa ya wanaume hata waliomo kwenye ndoa, kuzaa watoto ovyo na kuwatekeleza, huku jamii ikiwapa majina mabaya watoto hao kwa kuwaita 'watoto wa mtaani'.

Alisema ifike mahali, Katiba iseme wazi na uwepo utaratibu wa kuwatambua watoto wanaozagaa mitaani na waliotelekezwa na baba zao, huku wakikosa huduma muhimu ikiwamo huduma za lazima na kwamba sheria na haki isidhulumiwe kwa mtoto wa Kitanzania.

"Kila siku madai Katiba mpya, Katiba mpya, iliyopo mbona hamwifuati. Sehemu gani wamesema kutakuwapo watoto wa mtaani. Tunafahamu duniani na Katiba inasema binadamu wote ni sawa, wana haki sawa, mbona watoto mnawaita wa mtaani'," alisema.

"Kwani mitaa ndio imezaa watoto hawa. Tuache unafiki na ubinafsi, watoto watambuliwe baba, mama zao hata kama ni wangu (Butiku), unafiki wangu usifanye mtoto akose haki, tunajenga taifa la aina gani," alihoji kiongozi huyo ambaye aliwahi kushika nyadhifa tofauti, ikiwamo Ikulu, Serikali ya awamu ya kwanza.

Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ilisema kuna haja ya kuchukua hatua na kutafuta kwa kina chanzo nini cha kasi ya kuvunjika kwa ndoa nchini, ikieleza kushtushwa na kasi ya kuvunjika kwa ndoa nchini.

Ilisema, chanzo kikubwa ni kumomonyoka kwa maadili, huku Mkoa wa Dar es Salaam pekee ndoa ni zaidi ya 300 zikivunjika kwa mwezi.

"Tumepata hesabu (ya ndoa kuvunjika) kwa mfano Dar es Salaam pekee yake zaidi ya ndoa 300 kwa mwezi zinavunjika. Hili tunaona ni tatizo kubwa ni janga. Sisi kama kamati tunaona haja kubwa ya kuishauri serikali kuona jinsi gani kuchukua hatua kwa ajili ya kupambana na hali hii iliyopo,"alisema Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo.

Mtaalamu wa Ustawi Jamii na Mshauri na Masuala ya Familia, Malezi na Makuzi ya Watoto na Malezi ya Vijana, Joseph Kayinga, aliimbia Nipashe jana kwamba, malezi ya watoto ya mzazi mmoja yanaongezeka na kwamba imekuwa chanzo cha tatizo la mtoto kuathiriwa kisaikolojia.

# Samia, Hichilema wakubaliana kuboresha bomba la TAZAMA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, wamekubaliana kuharakisha uboreshaji wa bomba la mafuta la Tanzania na Zambia (TAZAMA) ambalo limedumu kwa miongo mitano sasa.

Bomba hilo lenye urefu wa zaidi ya kilomita 1,000 limekuwa likifanya kazi tangu mwaka 1968 huku likisafirisha zaidi ya tani milioni moja za mafuta ghafi kwa mwaka kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Ndola, Zambia.

Katika taarifa iliyopatikana kwenye ukurasa wake wa Facebook, Rais Hichilema, alisema amekutana na Rais Samia pembeni ya mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi za Afrika unaofanyika Addis Ababa, Ethiopia huku bomba hilo la mafuta likiwa ajenda yao kuu.

"Kikao chetu kilijikita kwenye kuimarisha uhusiano baina ya nchi zetu katika eneo la biashara na uwezeshaji, uwekezaji katika nishati baina ya mataifa yetu mawili," alisema.

Haikande alisema ajenda kuu kwenye mkutano wake na Rais Samia ilikuwa bomba la mafuta la TAZAMA ambalo wamekubaliana likarabatiwe na mifumo yake ya usalama.

"Bomba hili ni hazina kubwa kwa taifa la Zambia ikizingatiwa kwamba nchi yetu haizalishi mafuta yake yenyewe na inategemea kuagiza mafuta yote kutoka mataifa ya Ulaya na Mashariki ya Kati kupitia Bandari ya Dar-es-Salaam," alisema.

Naye Rais Samia kwenye ukurasa wake wa Facebook, aliandika kuwa alifanya mazungumzo na Rais wa Zambia na kumweleza kwamba Tanzania ilikuwa makini kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa maslahi mapana ya nchi hizo mbili.

Zambia inahitaji lita milioni moja za mafuta kwa siku na katika taarifa yake ya hivi karibuni, Waziri wa Nishati wa Zambia, Peter Kapala, alisema serikali itajitahidi kudhibiti ongezeko la mafuta na kuwahakikishia wasafirishaji kwamba biashara yao haitaathiriwa kwani huduma yao inategemea zaidi uwapo wa bomba hilo.

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Herman Kasekende, wakimwagilia maji mti baada ya kuupanda katika Shule ya Msingi Shukuru Kawambwa, Kata ya Kiloma mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mbunge wa Bagamoyo, Mwalamu Mkenge. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wajeruhiwa na fisi wakienda shambani

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU saba wakazi wa Mtaa wa Bugosi, katika Halmashauri ya Mji wa Tarime wakiwamo watano wa familia mbili tofauti, wamelazwa hospitalini baada ya kujeruhiwa na fisi.

Watu hao Francis Siongo, Joseph Siongo, Seta Saro, Anna Saro, Slia Saro na Mang'enyi Chacha, walikutwa na mkasa huo wakiwa njiani kwenda shambani kulima.

Wakisimulia tukio hilo wakiwa wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya Tarime juzi, baadhi ya majeruhi hao walioweza kuzungumza walisema fisi huyo aliwavamia alfajiri wakiwa njiani.

Francis Siongo na Seta Ngoncho walisema kwa nyakati tofauti kuwa mkasa huo uliwakuta saa 11:00 jana wakienda kwenye mashamba yao yaliyoko Nyandoto.

"Tulikuwa na jembe la ng'ombe na wengine walikuwa na majembe ya mkono, ghafla alijitokeza fisi na kutaka kushambulia mifugo yetu na hapo ndipo tulijaribu kujihami kupambana na fisi huyo huku tukipiga kelele," alisema Siongo.

"Watu waliokuwa jirani na sisi walijitokeza kutoa msaada lakini fisi huyo alitujeruhi vibaya kwa kutung'ata mikono, usoni na sehemu mbalimbali za miili yetu kama mnavyotuona hapa tumelazwa.

"Mama yetu Anna Saro amejeruhiwa vibaya kwa kung'atwa pua, mdomo na mikono na sisi hapa mnatuona tulivyojeruhiwa vibaya na fisi huyo wa ajabu," alisema Seta.

Diwani wa Nyamisangura, Thobias Ghati, alisema wananchi hao wamejeruhiwa vibaya na fisi na kwamba baada ya tukio hilo, wananchi walijitokeza kupambana na fisi huyo kwa kushirikiana na askari polisi na kufanikiwa kumuua. "Tunawaombea wenzetu hawa wapate nafuu ili kurejea kujenga taifa na tunawaomba wananchi kushiriki katika ulinzi shirikishi katika kila mtaa na kujitokeza mara wanaposikia kuna tatizo lolote linalojitokeza katika maeneo yao.

Pia aliwaomba wananchi hao kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Tarime, Dk. Innocent Kweka, alithibitisha kuwapokea na kuwalaza majeruhi hao saba.

"Leo (jana) Jumanne Februari 21 asubuhi, tumwapokea majeruhi saba waliokuwa na majeraha mbalimbali kwenye miili yao yaliyotokana na kung'atwa na fisi kichwani, mikononi, miguuni, puani na mdomoni.

"Majeruhi watano wanaendelea vizuri katika hospitali yetu ya wilaya lakini wawili, mmoja wa kiume na mmoja wa kike tunawahamishia leo (jana) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Musoma kupata matibabu zaidi," alisema Dk. Kweka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) Geofrey Sarakikya, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo la watu saba kujeruhiwa na fisi.

"Watu saba wamejeruhiwa na fisi wakati wakienda mashambani kulima alfajiri na wamelazwa hospitali ya wilaya wakipatiwa matibabu. Fisi aliyesababisha madhara hayo ameuawa na wananchi walipopambana naye.

"Tunawahimiza wananchi kuwa makini na kulinda familia wakiwamo wanafunzi kutoondoka usiku wa giza kwenda shuleni wawe wanasubiri kunakucha ili kuepuka wanyama hao hatari," alisema Kamanda Sarakikya.

## Utaratibu mpya kuingia stendi Magufuli waanza

**Na Elizabeth Zaya**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ubungo imetangaza kuanzisha utaratibu mpya wa ukataji wa tiketi kwa njia ya kadi katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli kilichoko Mbezi Luis, Dar es Salaam.

Imesema itatumia mfumo huo kwa kila abiria badala ya mfumo uliokuwa unatumika awali wa kukata risiti za karatasi na kwamba utaratibu wa kuingia kwa kadi utakuwa kwa kila abiria anayeingia iwe ana tiketi ya kusafiria au laa.

Kaimu Ofisa Habari wa Manispaa ya Ubungo, Joina Nzali, alisema jana kuwa tayari mfumo huo umeanza kutumika tangu juzi.

"Mfumo huo mpya wa kadi za N-CARD umeanza rasmi. Kwa hiyo kila abiria ambaye tayari alikuwa na kadi hiyo akiitumia kwenye maeneo mengine, yakiwamo Uwanja wa Taifa (Uwanja wa Mkapa) au Magogoni Feri, ataendelea kutumia kadi hiyo hiyo. Kwa abiria ambaye si mkazi wa Dar es Salaam na anatumia mara moja kituo hicho cha mabasi, atapatiwa kadi ya kutumia mara moja," alisema Nzali.

Alisema awali utaratibu uliokuwapo ni kwamba kwa abiria ambaye alikuwa tayari na tiketi ya gari ya safari alikuwa akiruhusiwa kupita bila kulipa ushuru, lakini kwa sasa kila mtu anayeingia ndani ya kituo atalipia hata kama ana tiketi.

Kupitia mfumo huo, alisema wanakadiria kukusanya mapato ya Sh. bilioni 5.4 kwa mwaka huku kwa mwezi ikikadiriwa kukusanya Sh. milioni 420 wakati mfumo wa ukataji tiketi wa zamani kwa mwaka 2021/22 walikusanya Sh. bilioni 3.7 pekee.

Pia alisema hatua ya matumizi ya N- CARD inalenga kupunguza foleni hasa wakati wa asubuhi na kwamba kuna abiria na wasindikizaji wengi katika eneo hilo.

Mmoja wa watumiaji wa stendi hiyo, akizungumza na Nipashe kuhusu mfumo mpya, Shukuru Manyama, alisema mfumo huo ni mzuri katika kudhibiti upotevu wa mapato lakini akashauri kwamba ni vyema ungelenga watumiaji wanaoingia humo ambao si wasafiri.

"Huu ni mfumo mzuri na utasaidia halmashauri kukusanya mapato mengi kwa sababu upotevu wa hapa na pale utapungua lakini ungelenga wale wanaoingia humo ambao siyo wasafiri au wale ambao hawajakata tiketi za kusafiri.

"Nasema hivyo kwa sababu abiria anapokata tiketi kwenye basi kwa ajili kusafiri, tayari amekuwa amekatwa kodi, sasa kumtoza ushuru tena unakuwa unamtoza kodi mara ya pili ambayo sidhani kama ni sahihi. "Utaratibu huo waliouanzisha waendelee nao, lakini iwe ni kwa wale ambao hawana tiketi pekee kama ambavyo walikuwa wanafanya awali kabla ya mfumo huo mpya," alisema.

Mtumiaji mwingine aliyejitambulisha kwa jina moja la Richard, alisema: "ushuru...ushuru...ushuru. Nchi ina majaribu hii. Yaani unapokata tiketi nauli unayolipa tayari ina ushuru ndani yake maana basi hilo lazima lilipe ushuru, sasa abiria kwa nini abebeshwe huu ushuru wa kuingia stendi.

"Kwa hali hii tutapanda kwenye vituo vya mawakala wala hatuendi huko kwa Magufuli."

Naye Erick Amani alisema shida si kutumia mfumo wa kadi isipokuwa tatizo ni kwa nini hiyo fedha ya getini wasingeijumulisha humo humo kwenye nauli kama ambavyo inavyofanyika kwenye kupanda kivuko?

# Mwanafunzi darasa la nne akutwa amejinyonga

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWANAFUNZI wa darasa la nne wa Shule ya Msingi Kambarage, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Tatu John, amekutwa amejinyonga kwa kutumia kamba kwenye chumba cha kulala nyumbani kwao.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mkoani B, Shabani Rashid, alisema jana kuwa alipokea simu kutoka kwa mjumbe wa mtaa wake, akimweleza kuwa kuna mtoto amejinyonga ndani ya nyumba. Rashid alisema majira ya saa tisa kasoro alasiri Februari 19, mwaka huu, alipigiwa simu na mjumbe huyo na kabla hajaenda alitoa taarifa polisi ili wafike kwenye eneo la tukio.

Alisema alipofika alikuta wafiwa wako na mjumbe, ndipo walipoingia ndani ulipokuwapo mwili wa marehemu na kukuta akiwa ameingiza kichwa ndani ya kamba ya chandarua ambayo imefungwa dirishani mkono wa kulia na kushoto.

"Eneo la tukio ni dirishani kwenye chumba ambacho walikuwa wanalala watoto na tulimkuta Tatu amepiga magoti. Polisi walifika wakapiga picha na kuchukua alama zao kisha wakaondoka na mwili kuupeleka Hospitali (Teule ya Rufani ya Mkoa) ya Tumbi kwa ajili ya uchunguzi zaidi," alisema. Alisema wananchi wanaoishi Mkoani B, kutokana na tukio hilo, wamepata taharuki kwa mtoto wa miaka kumi darasa la nne kuchukua uamuzi wa kujinyonga.

Rashid aliwashauri wazazi kujenga ukaribu na watoto wao pamoja na kuuimarishe ulinzi katika familia hasa kwa watoto ili kujua vikwazo wanavyokutana navyo na kuvitatua kabla havijasababisha madhara.

Baadhi ya majirani ambao hawakutaka kutaja majina, walisema tukio hilo limegubikwa na utata kutokana na mazingira yake ambayo inadaiwa Tatu alikutwa amepiga magoti baada ya kujinyonga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo ambalo alisema uchunguzi unaendelea.

Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Tumbi ukisubiri taratibu za mazishi.

# Serikali yataja mikakati kupambana na surua

**Na Romana Mallya**

WAKATI idadi ya watu waliougua ugonjwa wa surua ikifikia 667, wakiwamo watoto chini ya umri wa miaka mitano, serikali imesema katika kuudhibiti, inaendelea kuyaainisha maeneo ambayo hayajapata chanjo au kuikamilisha ili wapewe.

Jumapili, Nipashe ilimnukuu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, mkoani Katavi, Dk. Martin Lohay, kuhusu kuwapo kwa vifo vya watoto 12 chini ya umri huo na watoto 646 wakiambukizwa katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Desemba, mwaka jana.

Taarifa iliyotolewa jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, iliyokuwa ikifafanua mwenendo wa ugonjwa huo, ilisema katika kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Februari, mwaka huu, wagonjwa waliothibitika kuwa na maambukizi wamefikia 667.

"Hadi sasa kuna vifo 12 kutoka Wilaya ya Mlele, Halmashauri ya Mpimbwe, vifo 10 kati ya hivyo vimetokea ngazi ya jamii, vilichangiwa na watoto waliougua kutofikishwa katika vituo vya kutolea huduma mapema," alisema. Alisema kati ya wagonjwa waliothibitika, 305 walikuwa na umri chini ya miaka mitano na wapo wenye umri wa zaidi ya miaka 18.

"Asilimia 59 ya wagonjwa waliothibitika kuwa na maambukizi hawakuwa wamepata chanjo yaani dozi ya kwanza ya surua, wakati asilimia 21 walikuwa hawajakamilisha chanjo yaani kupata dozi ya pili ya surua," alisema.

Alisema mikoa yenye wagonjwa wengi ni ile ya ukanda wa Pwani yaani Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Mtwara na Lindi.

Prof. Nagu alisema mikoa ambayo imedhihirika japo kwa kuwa na wagonjwa wachache ni Tabora, Kagera, Mbeya, Arusha, Katavi, Kigoma, Rukwa, Simiyu, Shinganya, Dodoma, Geita, Mara, Ruvuma na Njombe. "Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya kuzuia na kupambana na ugonjwa wa surua tangu kutangazwa kwa mlipuko huu kwa kuimarisha utoaji wa chanjo, elimu kwa jamii, ufuatiliaji wa wahisiwa kwa kuchukua sampuli na kuzipeleka maabara ya taifa ili zipimwe," alisema.

Prof. Nagu alisema katika kuudhibiti wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na wadau, inaendelea kuchukua hatua.

"Tunachukua hatua za kuimarisha maeneo yenye watoto wengi ambao hawajawahi kupata na kukamilisha chanjo ya surua-Rubella kwa kuwapatia kwa kushirikiana na watoa huduma ngazi ya jamii.

"Tunaimarisha utoaji wa chanjo kwa watoto wote maeneo yaliyobainika kuwa na watoto wengi hawajapata au kukamilisha ratiba zao za chanjo hii ni pamoja na mikoa yote iliyobainika kuwa na mlipuko wa ugonjwa, hili hufanyika nyumba kwa nyumba," alisema.

Pia alisema wanaendelea kutoa msisitizo na hamasa kuhusu huduma za chanjo za kila siku.

Alisema awamu ya kwanza ya mchakato wa kuongeza kiwango na kasi ya kutoa chanjo kwa kutekeleza kampeni ndogo ya siku tano kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Lindi, Mtwara, Arusha na Katavi iliyoanza Desemba mwaka jana, linatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Alisema awamu ya pili itaendelea kwenye mikoa iliyosalia ambayo imeonyesha kuwa katika hatari ya maambukizi.

Alisema Septemba mwaka jana, wizara ilitoa tamko kuwapo kwa ugonjwa huu kwa baadhi ya halmashauri ambapo mikoa ambayo watoto wengi ambao hawajapata chanjo ilikuwa ni Kigoma, Kagera, Mara, Songwe, Manyara na Mbeya. Alisema mikoa ambayo haikukamilisha chanjo ilikuwa ni Tabora, Dar es Salaam, Arusha, Geita, Rukwa, Shinyanga, Manyara, Pwani, Singida, Ruvuma, Dodoma, Kigoma, Morogoro , Lindi, Songwe, Mtwara, Katavi, Iringa na Mbeya.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Araman Benoite (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa, wakikabidhi mtungi wa gesi wa Oryx kwa mmoja ya wanawake wajasiriamali jijini Tanga, lengo likiwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Jumla ya wanawake wajasiriamali 600 katika jiji hilo walipewa bure mitungi na majiko ya kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakazi Kigamboni wapata nafuu tozo kwa kuvuka Daraja Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umetekeleza kwa vitendo maagizo yaliyotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita ya kupunguza gharama ili kuwaondolea kero wananchi na watumiaji wa Daraja la Nyerere, Kigamboni, Dar es Salaam.

Hatua hiyo imekuja baada ya mfuko kuzindua rasmi mfumo wa NSSF 'Bridge Portal' ambao unawezesha mteja kununua bando la siku, wiki au mwezi ili kupita na chombo cha moto katika daraja hilo.

Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa NSSF, Donald Mhaiki, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na NSSF, zilipitia gharama za tozo za darajani kwa vyombo vya moto vinavyopita katika daraja hilo na kufanya punguzo kubwa la tozo.

Mhaiki amesema punguzo hilo lilianza kutumika rasmi Mei, mwaka jana na mfuko ulikuja na punguzo zaidi kwa kuanzisha mfumo wa bando. Kutokana na mfumo huo, mtumiaji wa daraja anaweza kupita kwa kulipia kwa siku, wiki au mwezi.

Alisema kabla ya kuanza kwa mfumo huo, mtumiaji wa daraja alikuwa anatumia wastani wa Sh. 90,000 kwa mwezi, lakini kwa kutumia mfumo huu hivi sasa mtumiaji wa daraja anatumia Sh. 35,000 kwa mwezi.

Mhaiki alisema mfumo huo unamwezesha mtumiaji kusajili chombo chake cha moto na kwa chombo ambacho hakijawahi kupita, mteja anatakiwa afike ofisi za NSSF zilizoko darajani hapo kwa ajili ya kusajili na hatimaye kununua bando. Kwa mujibu wa Mhaiki, chombo ambacho kimeshawahi kupita darajani angalau mara moja, mteja anaweza kusajili kupitia mfumo wa kielektroniki bila kulazimika kufika ofisi za NSSF.

Naye Emmanuel Masika, msimamizi wa Daraja la Nyerere, alisema mfumo huo wa bando umerahisisha upitaji wa darajani kwa maana ya kuondoa foleni na upitaji wake ni rahisi.

Meneja wa NSSF Mkoa wa Kigamboni, Judith Kebara, alisema huduma hiyo ni nzuri na ni fursa kwa wanachama na Watanzania kwa ujumla kwani vipato vinaenda kuongezeka, hali ya uchumi inaenda kuimarika na inapunguza msongo wa mawazo.

# NDC yavutia uwekezaji maeneo 11 ya kimkakati

**Na Restuta James**

SHIRIKA la Taifa la Maendeleo (NDC), limeita wawekezaji wazawa na wa nje ya nchi, wenye nia ya kuanzisha viwanda nchini kuwekeza mitaji yao kwenye maeneo 11 yaliyotengwa.

Eneo mojawapo kati ya hayo ni uzalishaji wa mpira na viwanda vya matairi ambalo linahitaji uwekezaji wa haraka, hivyo limewataka Watanzania kuchangamkia kilimo hicho katika mashamba ya NDC kwenye mikoa ya Tanga na Morogoro.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC, Dk. Nicolaus Shombe, alisema jana ofisini kwake, Dar es Salaam, alipozungumza na Nipashe kuwa shirika hilo lina maeneo ya uwekezaji kwenye viwanda vya dawa, chanjo, vifaa tiba, mbolea, viuatilifu, makaa ya mawe na chuma.

Alisema eneo lingine ni uzalishaji wa matairi, vipuri vya magari na mitambo, nishati, majengo na bandari kavu.

Dk. Shombe alisema NDC inakusudia kufufua kiwanda cha magurudumu cha General Tyre cha jijini Arusha.

"Biashara ya matairi ni kubwa na hapa ni sehemu tunayohitaji mwekezaji wa haraka," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Shombe, kiwanda hicho kinahitaji mfumo wa teknolojia ya kisasa ili kianze uzalishaji kwa kuwa majengo na miundombinu mingine iko katika hali nzuri.

"Tunataka tuanze kuzalisha walau matairi ya bodaboda na bajaji. Unaweza kuona kwamba matairi ni biashara kubwa ambayo mwekezaji yeyote ana uhakika wa kurudisha mtaji ndani ya muda mfupi," alisema.

Dk. Shombe alitaja fursa zilizopo katika eneo la viwanda Kibaha, mkoani Pwani kuwa ni uzalishaji wa dawa za binadamu, vifaa tiba, mbolea, viuatilifu na nguo.Alisema katika eneo hilo, kuna mwekezaji mbia anayezalisha chanjo za wanyama pamoja kiwanda cha NDC kinachozalisha dawa ya kuua mazalia ya mbu.

"NDC tumeanza kuzalisha viuadudu vya mazao kama pamba, mboga na matunda, majaribio yamefanyika na matokeo ni mazuri sana, tunategemea kuzalisha mbolea rafiki kwa mazingira na dawa za mimea zisizo na kemikali," alisema.

Alisema pamoja na uzalishaji unaofanywa na NDC, eneo hilo linahitaji wawekezaji wakubwa na wadogo wa viwanda.

Alisema katika eneo hilo, kuna kiwanda cha kuunganisha malori na magari makubwa na kwamba fursa zaidi zilizopo katika eneo hilo ni uwekezaji wa viwanda vya usindikaji wa vyakula na nguo.

Mkoani Pwani, alisema kuna mradi mwingine ambao uko karibu na bandari kavu ya Kwala kwa ajili ya uwekezaji wa chuma na nondo na kwamba miundombinu yote muhimu ipo akitaja kuwa linafikika kwa reli ya kisasa, barabara na kuna umeme mkubwa.

HABARI KITAIFA

# Ujenzi bomba la mafuta sasa waiva

**Na Frank Monyo**

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imekabidhi rasmi kibali cha ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa Kampuni ya EACOP Tanzania kutoka Kabaale - Hoima nchini Uganda kwenda Chongoleani mkoani Tanga. Makabidhiano hayo yalifanyika jana Salaam na kuhudhuriwa na wakuu wa mikoa minane ya Tanzania Bara linakopita bomba hilo. Mikoa hiyo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.

Mradi huo una urefu wa kilomita 1,443 kati ya hizo, 296 ziko Uganda na kilomita 1,147 zipo Tanzania. Lengo la mradi huo ni kuwezesha mafuta yatakayozalishwa Uganda kusambazwa katika soko la ndani na sehemu inayobaki kuuzwa nje kwenye soko la kimataifa kupitia bomba la mafuta.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo, Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema Tanzania na Uganda zimeunganishwa na barabara, njia ya umeme lakini kwa sasa zitaungwanishwa chini ya ardhi kupitia bomba hilo ambalo mradi wake unatarajiwa kutoa zaidi ya ajira 1,000.

"Kwa nchi yetu sisi kuwa wenyeji wa bomba la mafuta kumeongeza nguvu na ushawishi katika ukanda huu wa Afrika kama ilivyokuwa kwenye bomba la TAZAMA (Tanzania na Zambia). Ramani mpya ya dunia ukiichora sasa hivi ukachukua miundombinu inayounganisha nchi kwa nchi, mradi huu wa kusafirisha mafuta kutoka Uganda kuja Tanga utaongezeka kwenye mchoro wa ramani ya dunia," alisema. Kuhusu ujenzi wa bomba hilo hasa utunzaji wa mazingira, Mkamba alisema kumekuwa na mazungumzo mengi kuhusu mradi huo kwamba haufai kujengwa na hata Bunge la Umoja wa Ulaya liliweka zuio ingawa halikuwa na meno ya kuzuia.

"Wenzetu ambao wanaamini kwamba hatustahili kuvuna hizi rasilimali, wametumia njia nyingi kuweka shinikizo mradi huu usiendelee," alisema Mkamba.

Alisema si kweli kwamba mradi huo utakiuka haki za binadamu na utunzaji wa mazingira kwa kuwa imefanyika tathmini ya kimazingira kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

"Sehemu ambayo bomba litapita patafunikwa kwa kupandwa miti juu yake. Pia kulikuwa na maneno kuhusu haki za binadamu, kwamba kutakuwa na shida na kwamba labda watu wataondolewa kwa nguvu katika maeneo yao.

"Watu 9,898 waliguswa na mradi huu kati yao 390 ndio ardhi yao itachukuliwa kwa ajili ya kupitishwa bomba na watu hao wapewa fursa ya kuchagua kujengewa nyumba au kulipwa fedha. Asilimia 85 wameachagua kujengewa nyumba na wamejengewa nyumba bora na za kisasa. Kwa wale bomba lilipita katika maeneo yao walelipwa fidia ya Sh. bilioni 29 na TPDC (shirika la maendeleo ya Petroli Tanzania)," alisema.

Makamba aliiomba EWURA kusimamia na kuweka uwazi wa fursa za ajira zinazotokana na mradi wa bomba hilo.

Alisema mradi huo katika kazi za awali, umetoa ajira 200 kwa Watanzania na kampuni 100 za Kitanzania zimepata kazi katika kipindi hicho. Watanzania wameelimishwa kuhusu mradi huu na manufaa yake.

## Wawekezaji wakaribishwa kuwekeza mradi wa bil. 236/-

**Na Romana Mallya**

WAWEKEZAJI wazawa na wa nje ya nchi wamekaribishwa kuwekeza katika mradi mkubwa wa Dola za Marekani milioni 100 (zaidi ya Sh. bilioni 236) unaotekelezwa eneo la Nungwi Mashariki, mjini Zanzibar wenye lengo la kukuza utalii visiwani humo.

Mradi huo wa makazi ambao umesajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 36 na utatoa fursa kufanya utalii kwa kutembelea visiwa vya karibu kujua historia na utamaduni. Mwendelezaji wa mradi huo, Squid Limited Zanzibar ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, George Alexandru, alisema jana kuwa ujenzi wake ulianza mwishoni mwa mwaka jana na kwamba awamu ya kwanza itahusisha nyumba 238.

Alisema kwa uwekezaji wa awali, mwekezaji anaweza kuwa mmiliki wa mradi kwa Dola za Marekani 50,000 (sawa na Sh. milioni 118).

"Kwa mujibu wa marekebisho namba 10 ya Zanzibar Condominium Act ya 2010, baada ya ununuzi uliofanikiwa, mnunuzi atapewa hati ya umiliki ya kukodisha kwa miaka 99. Muda wa kukodisha kwa kawaida hutolewa kwa awamu za miaka 33 kila moja. "Wale wanaowekeza katika mradi huu watanufaika kwa punguzo la kodi kama wakazi na makadirio ya kupata faida ya uwekezaji ya asilimia 12 kila mwaka huku malipo ya faida yakitegemewa kuanza kupatikana baada ya miaka saba, kwa mujibu wa mwendelezaji wa mradi huo," alisema.

Alisema baada ya kuwekeza katika mradi huo ujulikanao kama The Ocean Pearl Zanzibar, iwe kwenye majengo ya studio, duplex au villa, mwekezaji ana hiari ya kuikodisha na kusimamiwa na kampuni mahsusi ya kutoa huduma za ukarimu.

Pia alisema huduma nyingine kwenye mradi huo ni bwawa la kuogelea, fukwe za bahari, chakula na safari kwenye visiwa vya karibu, historia na utamaduni.

"Mradi wenye hadhi ya nyota tano utakuwa na huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na migahawa kadhaa, baa pamoja na baa kwenye gati, klabu ya usiku, duka la chokoleti, spa na eneo la mazoezi (gym), na mabwawa ya kuogelea," alisema.

Awamu ya kwanza ya mradi, alisema inatarajiwa kujengwa kwenye eneo la zaidi ya mita za mraba 130,000 itakayojumuisha kituo cha biashara wakati eneo kubwa litakuwa maalum kwa mabwawa ya kawaida na bustani huku ujenzi wa eneo la kutua helikopta unatarajiwa kuwezesha kufikika kwa anga.


SALAMU ZA PONGEZI

ACB
AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako




Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Akiba Commercial Bank Plc wanatoa pongezi za dhati kwa Mkurugenzi huru wa bodi, Profesa Josephat Daniel Lotto kwa kuchaguliwa kuwa Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Tunamtakia mafanikio mema kwenye majukumu yake mapya na tunaamini kuwa uwezo wake, ufanisi na weledi vitaleta mafanikio makubwa kwa Chuo cha IFM.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mpango wa CBE kuwaandaa wahitimu kujiajiri mwafaka

**CHUO** cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeeleza mikakati yake ya kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana kwa kuanzisha mpango wa masomo ya uanagenzi na atamizi.

Kupitia mpango huo, wahitimu watapata ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira pamoja na kujiajiri.

Mkakati huo umekuja kwa wakati mwafaka hasa ikizingatiwa kuwa wahitimu wa vyuo vikuuu wamekuwa wakizunguka katika ofisi mbalimbali kwa ajili ya kusaka ajira za ofisini huku wengi wakikosa na kubaki nyumbani.

Lakini sasa mpango huu ni mahususi kwa kuwa unawaandaa vijana kujiajiri na kuajiri wenzao.

Ni ukweli kwamba nafasi za ajira serikali na sekta binafsi ni chache licha ya kwamba wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka kutokana na kuhitimu elimu ya juu ya vyuo vya kati wamekuwa wakiongezeka.

Kutokana na ukweli huo, serikali mara kadhaa imekuwa ikitamka kwamba haiwezi kuajiri wahitimu wote hivyo ni muhimu waandaliwe kuwa na uwezo wa kufanya biashara au kuendesha kampuni zao.

Kadhalika sekta binafsi nayo haiwezi kuajiri wahitimu wote wanaomaliza elimu ya juu.

Sababu kubwa ya kufanya hivyo, kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, ni kasi inayoongezeka ya mabadiliko ya kiteknolojia katika nyanja za biashara na uchumi ambayo imekuwa chachu kwa chuo kuwaandaa wahitimu wanaoendana na mabadiliko hayo.

Katika kufanya hivyo, amesema CBE imejielekeza zaidi kusaidia katika kutoa mafunzo kwa wahitimu wenye ujuzi wa biashara kwa uchumi wa Tanzania.

Hatua hiyo pia imetokana na chuo kutambua kuwa maendeleo ya rasilimali watu wenye ujuzi kwa uwezeshaji wa vijana, tija na ufanisi katika jamii unategemea wakufunzi wenye ujuzi na uzoefu na ubora wa taasisi za mafunzo.

Kwa mantiki hiyo, mafunzo ya uanagenzi yana msingi wa mafunzo kwa vitendo kwa kushirikiana na mahali halisi pa kazi ambapo mwanachuo hutumia nusu ya muda wake chuoni na nusu kwa mwajiri ambapo hupata fursa ya kujifunza kwa vitendo mambo ambayo tayari amekwisha jifunza kwa nadharia.

Hatua iliyochukuliwa na CBE ni ya kupogezwa na kuigwa na vyuo vingine kwa kuhakikisha vinabadili mitaala yao na kuwatengeneza wahitimu wanaoweza kujiajiri na kuajiri wengine wanapohitimu masomo yao.

Ni dhahiri kwamba uamuzi huu, kimsingi utaleta mabadiliko kwenye fikra za vijana kwa kujiajiri zaidi badala ya kusubiri kuajiriwa wanapomaliza elimu ya ngazi yoyote.


Pia uamuzi huu ni dira kwa vyuo vingine kubadili mifumo ya taaluma vinazotoa na kujielekeza zaidi kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kutengeneza ajira kwenye kampuni watakazoanzisha.

Suala hilo haliangazii watu kujiajiri na kuajiri wengine tu bali linapanua wigo wa sekta binafsi ambayo ni mhimili mkubwa katika ukuaji wa uchumi na pato la taifa kwa ujumla.

Hii ina maana kwamba iwapo kampuni nyingi zitaanzishwa kutokana na wahitimu kujiajiri, Watanzania wengi zaidi wataondokana na umaskini wa kipato pamoja na kuongeza makusanyo ya serikali yatokanayo na kodi mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuanze kuwekeza kilimo hata mijini

Na Mwandishi Wetu

**MWAKA** 2023 unapoanza inabainika kuwa mataifa mengi ya Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara hayana chakula cha kutosha. Tena moja ya sababu ni uharibifu wa mazingira unaoleta uhaba wa mvua, ukame, mafuriko na wadudu waharibifu mashambani.

Tanzania ni miongoni mwa mataifa hayo lakini haina uhaba mkubwa wa chakula japo gharama za chakula ziko juu kwenye maeneo mengi hasa mchele na unga wa mahindi.

Kadhalika kitoweo kama dagaa, samaki, nyama, kuku wa kienyeji vikiwa havishikiki.

Mambo ni magumu zaidi mijini kwani kuna idadi kubwa zaidi ya watu wanaoishi wakitegemea vyakula vinavyozalishwa vijijini au mashambani mikoani.

Kadhalika watu hao wengi wanaoishi mijini hawajishughulishi na kilimo hata kwa kiasi kidogo ikiwamo cha mboga zinazozalishwa kwenye makopo au viroba nyumbani.

Ni wakati sasa wa kuhamasisha wakazi wa mijini kupenda kulima hata mboga za kienyeji na kufuga ili kuwawezesha kula lakini kupata kipato kutokana na ukweli kuwa familia nyingi mijini hula na huhitaji mboga za majani kwa wakati wote.

Katika kilimo hicho changamoto mojawapo watu wanayoweza kukutana nayo ni ukosefu wa mbegu za mboga au mazao ya kienyeji hivyo serikali na wadau wa kilimo zikiwamo asasi za kiraia (CSO) za kitaifa na kimataifa zilione na kulishughulikia.

Lakini, wakati mwingine mbali na kukosa mbegu na hamasa kuwa familia zizalishe mboga zake zenyewe, ukosefu wa maarifa kuhusu mbinu zinazohitajika kufanya kilimo cha mboga na matunda mijini kiwe endelevu, nalo ni tatizo.

Kwa hiyo, ili kupambana na njaa na kuwezesha wakulima wadogo mijini hasa familia kujitosheleza kwa chakula hasa mboga, matunda na ufugaji wa wanyama wadogo kama kuku, bata, sungura na simbilisi serikali ianze kuhimiza sasa na kushirikiana na wananchi kubadili maisha yao na kupunguza njaa.

Jopo la Kimataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, linaeleza kuwa kuna changamoto ya hali ya hewa inayosababisha ongezeko kubwa la viuatilifu na visumbufu kwenye lakini hilo halizuii kutumia rasilimali na maarifa ili kupunguza mahitaji ya chakula yanayowakabili watu wengi.

Ni wazi kuwa iwapo sembe inauzwa ghali au mchele, unga wa ngano na kitoweo kama samaki, dagaa na nyama, familia ikiwa na kuku, bata, sungura au simbi inapunguza mahitaji ya kununua kitoweo kwa vile kinatoka nyumbani.

Gharama inaweza kuwa kwenye nafaka, mafuta na mahitaji kama sukari lakini mboga, matunda na kitoweo kikatoka nyumbani.

Wananchi wanaweza kufundishwa teknolojia ya kufuga na kulima kisasa kwenye eneo dogo. Maarifa hayo yatahitaji kuwapa watu maelekezo ya kujenga miundombinu kulingana na ardhi yao.

Kazi ianze na kuzalisha mbegu kwa kushirikisha wananchi hasa wanawake, kutoka maeneo mengi wakiwamo wale wanaomiliki maeneo ambayo ni rahisi kufanya kilimo.

Ni wazi kuwa kilimo cha mboga za asili na matunda kama topetope, ndizi za kisukari, komamanga, matango pamoja na ufugaji wa wanyama wadogo kitaongeza pato la wakulima na kubadilisha hali ya afya ya wakazi wengi wa mijini.

Pamoja na serikali kufikiria kuhusu mbinu za kutoa mikopo kwa wanawake, vijana pamoja na watu wenye ulemavu iangalie pia kuhusu upandaji wa mimea na ufugaji wa wanyama wadogo.

Miradi ya kilimo na ufugaji na teknolojia au mafunzo watakayopata yasaidia waweze kufahamu masuala ya kutunza ardhi, kupanda mimea kwa zamu, kutengeneza mboji, kupima mchanga, kupanda miti shambani na matumizi endelevu ya maji.

Hii inamaanisha kuwa wakazi wa mijini wanaweza kufikisha utaalamu huo vijijini na kuibadilisha sura ya Tanzania ikawa bora zaidi na isiyo na njaa.

HABARI KITAIFA

# Mashahidi saba kujenga kesi kusafirisha dawa za kulevya

**Na Kulwa Mzee**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kusafirisha dawa za kulevya inayomkabili Hussein Hariri na wenzake, unatarajia kuita mashahidi saba na vielelezo vitano.

Hayo yalibainika jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati upande wa Jamhuri ukiwasomea washtakiwa maelezo ya mashahidi.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mkazi wa Mbezi, Benson Muro na Mkazi wa Magomeni Mapipa, Ramadhani Almas, ambao wote wanadaiwa kusafirisha gramu 1,001.17 za dawa za kulevya aina ya heroin.

Washtakiwa hao walisomewa maelezo hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mary Mrio na Wakili wa Serikali, Carolina Matemu.

Wakili Matemu alidai upande wa Jamhuri unatarajia kuwa na mashahidi saba pamoja na vielelezo mbalimbali wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo.

Alitaja baadhi ya vielelezo hivyo kuwa ni pamoja na dawa hizo za kulevya, magari mawili, ripoti ya Mkemia Mkuu wa Serikali na hati ya ukamataji mali.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa Machi 17, 2016 eneo la Kituo cha Mafuta cha Oil Com, Mbezi Beach, Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Inadaiwa washtakiwa hao walikutwa wakisafirisha kiasi hicho cha dawa za kulevya aina ya heroin kinyume cha sheria.

Pia inadaiwa washtakiwa walikamatwa na polisi baada ya kupata taarifa kwa msiri aliyewaeleza kuwa kuna mtu eneo la Mbezi anajihusisha na uuzaji wa dawa za kulevya, hivyo waliweka mtego ndipo walipowakamata.

Washtakiwa walirudishwa rumande hadi watakapoitwa Mahakama Kuu kwa ajili ya kesi kuanza kusikilizwa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi Binafsi ya kusaidia Sekta ya Kilimo ya PASS Trust, Yohane Kaduma, akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya "Kijanisha Maisha" kwa wadau wake wa ndani, jijini Dar es Salaam jana, ili kuelewa na kufahamu dhana inayotokana na mpango kazi wa kuhimiza kijani shirikishi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CBE yaanzisha programu wahitimu kujiajiri

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimesema katika kukabiliana na hali ya ugumu wa ajira duniani kimeanzisha mpango wa masomo ya uanagenzi na mpango atamizi ili kuwapatia wahitimu ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Lengo la kufanya hivyo ni kutatua tatizo la ajira lililopo nchini kwa kuwafanya wahitimu wa chuo waendane na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia katika nyanja za biashara na uchumi na kujiajiri baada ya kuhitimu.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kozi ambazo zitaanza kufundishwa Septemba, mwaka huu.

Alitaja baadhi ya kozi hizo kuwa ni astashahada ya msingi ya uchumi na fedha, astashahada ya msingi ya usimamizi wa usafirishaji, astashahada ya msingi ya ujasiriamali na ubunifu, astashahada ya msingi ya uongozi wa biashara, usimamizi wa kumbukumbu na kakavazi, astashahada ya msingi ya masoko kidijitali (digital marketing) na astashahada ya msingi ya masoko na utalii.

"Katika ngazi hii tunampokea mwanafunzi ambaye amemaliza kidato cha nne na kufaulu walau masomo manne. Hapa tunaanza kumpa elimu ya msingi katika fani husika," alisema.

Prof. Lwoga alitaja mafunzo mengine yaliyoanzishwa na chuo hicho kuwa ni ya stashahada katika uchumi na fedha, stashahada katika usimamizi wa usafirishaji, stashahada katika ujasiriamali na ubunifu, stashahada katika uongozi wa biashara, usimamizi wa kumbukumbu na makavazi, stashahada katika masoko mtandao, stashahada katika masoko kwenye utalii na usimamizi matukio.

Alisema kasi inayoongezeka kila mara ya mabadiliko ya kiteknolojia katika nyanja za biashara na uchumi yamekuwa chachu kwa chuo kuwaandaa wahitimu wanaoendana na mabadiliko hayo.

"CBE imejielekeza zaidi kusaidia katika kutoa mafunzo kwa wahitimu wenye ujuzi wa biashara kwa uchumi wa Tanzania. Chuo kinatambua kuwa maendeleo ya rasilimali watu wenye ujuzi kwa uwezeshaji wa vijana, tija, na ufanisi katika jamii unategemea wakufunzi wenye ujuzi na uzoefu, na ubora wa taasisi za mafunzo," alisema.

Profesa Tandi alisema Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa miaka 58 sasa kimekuwa kikitoa huduma bora katika jamii kwa kutoa elimu ya biashara kwa wajasiriamali, kutoa wahitimu wenye ujuzi kulingana na uhitaji wa soko na kutoa mafunzo na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Alisema ili kutoa mchango kwenye maendeleo ya viwanda na biashara katika ukuaji wa uchumi endelevu Tanzania, chuo kimekuwa kinabadili mitaala yake na kuongeza kozi mpya zinazoendana na kuendeleza uchumi, biashara na maendeleo ya viwanda.

Katika kukabiliana na mfumo wa elimu ya juu na kutoa wahitimu wasio na ajira Tanzania, alisema CBE imekuwa ikiongeza matarajio mengi kwa wahitimu kwa kuwapatia ujuzi unaohitajika na soko la ajira ikiwa ni pamoja na wahitimu wengi kujitegemea kwa kujiajiri.

## KABWELA Na Fadhili Mohammed



# Mwongozo wa upangaji makazi vijijini watolewa

**Na Munir Shemweta,**
MBEYA

ILI kuondokana na matatizo ya upangaji vijijini, serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeandaa mwongozo wa upangaji makazi na ujenzi wa nyumba vijijini.

Licha ya kwamba upangaji wa vijiji na ujenzi wa nyumba bora vijijni unapaswa kuhusisha watu wote, serikali imeona ni vyema kutoa mwongozo kwa kutumia lugha rahisi inayoeleweka kuelezea kanuni muhimu za kuzingatiwa na mamlaka na wana vijiji katika kupanga makazi ya vijiji bila kutegemea kutoka kwa wataalamu.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, katika kikao kazi cha kujadili na kuweka mikakati wa kukwamua urasimishaji makazi kilichofanyika mkoani hapo.

Dk. Mabula alisema miongozo iliyozingatiwa katika uandaaji mwongozo huo ni pamoja na uandaaji wa mipango kina ya makazi vijijini na mwongozo wa utoaji vibali vya ujenzi na usimamizi wa ujenzi wa majengo kwenye mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2018.

Alisema eneo la makazi la kijiji ni sehemu ya mpango wa jumla wa matumizi ya ardhi ya kijiji unaoainisha maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile makazi, biashara, taasisi, kilimo, misitu, malisho ya mifugo, huduma za jamii na miundombinu.

Pamoja na kuainishwa kwa matumizi mbalimbali kwenye vijiji, alisema maeneo hayo kwa muda mrefu yamekuwa hayapatiwi umuhimu na mamlaka za upangaji katika kuzijengea uwezo serikali za vijiji ili kuyaandalia mipango kina ya kusimamia ukuaji wake kama miji ya baadaye.

"Vitovu vya vijiji vinapaswa kupangwa ili kuwezesha jamii kuishi kwa njia ya usawa na kufanya shughuli zao katika mazingira bora na kuweza kutoa fursa za kutosha za ajira na mandhari mazuri ya kuvutia na kuchangia katika maendeleo ya ukuaji uchumi," alisema Dk. Mabula.

Hata hivyo, Dk. Mabula alisema kutokana na mwenendo huo, bado kuna jukumu kubwa la kupanga matumizi ya ardhi ya vitovu vya vijiji na hususan makazi ili kupunguza migogoro na kuhakikisha kwamba vijiji vinakuwa na milki salama, mazingira bora ya makazi na muunganiko wa shughuli nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi na hifadhi ya mazingira.

Kamishna wa Ardhi nchini, Nathaniel Nhonge, alisema, kwa muda sasa kumekuwa na majengo kutopangwa na hivyo kushindwa kuakisi taswira nzuri ya uendelezaji miji nchini.

Kwa mujibu wa Nhonge, makazi holela nchini yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na maeneo ya kutoka mamlaka za udhibiti kutofanya vizuri pamoja na kiasi cha fedha kinachotengwa kwa shughuli za upangaji. "Eneo lingine ni kutotengwa fedha za kutosha ili kutekeleza miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi suala alilolieleza linachangia miji holela na jambo hilo limesababisha wizara kuja na programu ya urasimishaji makazi," alisema Nhonge.



Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa mkoani Lindi, Ramadhan Matola (katikati), akizungumza katika kikao cha baraza la umoja huo, mjini Liwale juzi. Kulia ni Katibu wa CCM Mkoa, Barnaba Essau na Mwenyekiti wa UVCCM wa mkoa huo, Twaiba Mpako. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Amuua mama mdogo kwa kumcharanga mapanga

**Na Beatrice Shayo**

MKAZI wa Kijiji cha Kihabe Kata ya Unamikumbi mkoani Singida, Maritha Ally (65), amefariki dunia baada ya kucharangwa mapanga sehemu mbalimbali ikiwamo kichwani na mtoto wa dada yake.

Tukio hilo lilitokea Februari 18, mwaka huu wakati mama huyo akienda kuchota maji kisimani ndipo mtuhumiwa huyo alimvamia na kumcharanga mapanga.

Akizungumza na Nipashe, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Kihabe, Paulo Sinda, alisema mama huyo alikwenda kuchota maji majira ya saa 10 alasiri wakati wao wakiwa kwenye gulio la wakulima linalofanyika kila Jumamosi.

"Huyu mama wakati anakaribia kufika kusimani ndipo alipokutana na huo umauti kwa kucharangwa na mapanga na kijana ambaye ni mtoto wa dada yake huwa anamuita mama mkubwa," alisema.

Alisema wakati anarudi nyumbani majira ya saa 2 usiku wakasikia sauti ya yowe akafika katika eneo la tukio na kumkuta mwanamke huyo akivuja damu.

Sinda alisema mtuhumiwa huyo wakati anafanya mauaji hayo kuna watoto walimuona na waliogopa kutoa taarifa mapema hadi ilivyofika majira ya saa mbili usiku.

"Baada ya kufika eneo la tukio nilinyanyua simu nikampigia mwenyekiti wa serikali ya mtaa maana nilipigwa na butwaa kwa hiki nilichokiona alifika eneo la tukio, akatoa taarifa polisi ndipo walipofika saa 6 usiku," alisema.

Alisema polisi walivyofika waliendelea na upelelezi wao na kufika kwenye nyumba ya kijana anayetuhumiwa kufanya mauaji hayo na kumkosa.

Alisema mwili wa marehemu ulichukuliwa na kupelekwa nyumbani kwa marehemu na jana daktari alifika asubuhi kuuchunguza mwili na kuruhusiwa kuzikwa.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Kihabe, Zainab Mangaya, alisema tukio hilo limetokea katika mtaa wake na alipatiwa taarifa majira ya saa 3:30 na alivyofika alikutana na unyama huo.

"Huyo mama amecharangwa mapanga akiwa na ndoa yake kabla hajafika kisimani kwa sababu hatujakuta maji yalijomwagika palikuwa pakavu ila damu nyingi tulikuta imekauka," alisema na kuongeza:

"Maeneo ya kichwani amecharangwa sana hadi ubongo umetoka ukiangalia huo mgongo na usoni umekatwa katwa na kuna tundu kubwa mgongoni sijui alimtoboa na kitu gani," alibainisha.

Mangaya alisema mwili huo umezikwa jana (leo) na marehemu ameacha watoto saba na mume ambaye hawezi kutembea kutokana na kuvunjika mguu tangu mwaka jana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Mutabihirwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

"Huyu kijana alimvizia na kumkata na kitu chenye ncha kali wakati akienda kuchota maji hatuwezi kusema ni panga alitumia mpaka tumpate mtuhumiwa atueleze alitumia kitu gani kumuua mama huyo," alisema.

Kamanda Mutabihirwa alisema chanzo cha kifo hicho ni mgogoro wa ardhi na kwamba wanaendelea kumsaka mtuhumiwa ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

# Mwenyekiti ataka UVCCM kupigwa msasa kiutendaji

**Na Sabato Kasika,** LIWALE

VIONGOZI wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) mkoani Lindi, wametakiwa kuhudhuria katika madarasa ya elimu ya uongozi yatakayowawezesha kutambua mipaka ya kazi zao, ili kuepuka kuingiliana kwenye majukumu.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Lindi, Twaiba Mpako, wakati wa kikao cha baraza la vijana wa CCM mkoa wa Lindi kilichoketi mjini Liwale juzi.

Alisema iwapo viongozi wa vijana wakipata elimu ya uongozi, itawasaidia kutoingiliana kwenye majukumu na hivyo kuepusha migogoro ndani ya jumuiya hiyo na chama kwa ujumla.

"Ni muhimu viongozi wa vijana kutambua majukumu ya kila mmoja wenu ndani ya jumuiya akiwamo mwenyekiti, katibu, katibu hamasa na chipukizi kwa kuzingatia kanuni ya UVCCM," alisema Twaiba.

Alisema njia hiyo itasaidia, kila mmoja kuheshimu majukumu ya mwezake, ili kutaepusha migogoro ndani ya jumuiya hiyo na kuwataka kuwa na kanuni za umoja wetu na kuzisoma, ili waelewe majukumu yao.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti, baadhi yao wamekuwa wakiingiliana katika kazi, kitendo kinachoonyesha kuna haja kuhudhuria madarasa ya elimu ya uongozi, ili wapigwe msasa utakaowafanya watambue mipaka ya majukumu.

"Mwenyekiti ni msimamizi, lakini unaweza kukuta anageuka kuwa mtendaji wakati katibu yupo, halafu wengine hawajavunja makundi ya uchaguzi, hivyo wote hawana budi kuhudhuria madarasa ya elimu ua uongozi," alisema.

Alifafanua kuwa kila kiongozi wa vijana katika kata atahudhuria madarasa hayo yatakayopangwa katika kila wilaya, ili yawasaidie kujua majukumu yao ndani jumuiya na hata kwenye chama.

Katibu wa CCM Mkoa wa Lindi, Barnaba Essau, alisema chama kitatoa ushirikiano na ushauri, ili kufanikiaha madarasa hayo ya viongozi wa UVCCM.

"Hiyo ndio ahadi yetu kwenu, chama kitatoa ushirikiano na ushauri ili kufanikisha madarasa ya elimu ya uongozi, ambayo ni muhimu kwa vijana waliochaguliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi,"alisema Essau.

Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa, Ramadhan Matola, alisema viongozi hao wa vijana wakizingatia maelekezo ya mwenyekiti wao, watapata uzoefu wa kutosha kupitia madarasa ya elimu ya uongozi.

"Madarasa ya elimu ya uongozi yatawasaidia kujiamini na kujibu hoja za wapinzani kwa ufasaha kama ambavyo mwenyekiti wetu wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, anaelekeza," anasema Matola.





# Maofisa watendaji kata wakabidhiwa pikipiki

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MAOFISA watendaji kutoka kata nane za Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, mkoani Arusha, wamekabidhiwa pikipiki zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuwarahisishia utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi wa eneo hilo.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi pikipiki hizo, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema pikipiki hizo zitakuwa muhimu kwa watumishi hao kwa kuwa zitasaidia kumaliza tatizo la kutembea umbali mrefu kwa watendaji kuwafikia wananchi na utoaji wa huduma.

Alisema kata hizo nane ziko maeneo ya pembezoni na kwa sehemu kubwa ya maeneo ya kiutendaji maofisa hao hulazimika kutembea umbali mrefu kuwafikia wananchi ili kuwapatia huduma.

Hivyo aliwataka kutumia pikipiki hizo kwa ajili ya kazi iliyokusudiwa na serikali na siyo vinginevyo, huku akiwasisitiza kuzitunza na kuzithamini kwa kutambua kuwa ni mali ya umma.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwathamini watendaji wa kata, kwa kuwa wao ndiyo wanawahudumia wananchi moja kwa moja, hivyo mna deni la kwenda kuwatumikia watu na kutumia vyombo hivi vya kulingana na malengo yaliyokusudiwa na siyo mkavitumie kwa matumizi binafsi,"alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arumeru, Noel Severe, aliipongeza serikali kwa kutekeleza Ilani ya chama hicho kwa vitendo, kwa kuhakikisha watumishi wanapata vitendea kazi vitakavyorahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wananchi katika maeneo yao.

"Serikali inawategemea mmepata usafiri huu mkatumie muda mwingi kutatua kero na matatizo ya wananchi kwenye vijiji na vitongoji vyenu tena kwa wakati kwa kufanya hivyo tutafikia malengo ya serikali ambayo ndiyo maelekezo ya ilani," alisema.

Watendaji hao waliipongeza serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia usafiri kwa kuwa awali tatizo la kukosa chombo cha usafiri kwenye maeneo yao liliwasumbua na kukwamisha baadhi ya shughuli zao.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Oldonyosambu, Lomnyaki Ndiyogi, licha ya kuipongeza serikali alisema watumishi hao walikuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilomita 50 na walitumia zaidi ya saa nane kufanya kazi moja.

"Kupitia pikipiki hizi zinakwenda kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wetu, kwa kuwa awali tulikuwa tunafanya kazi kwa siku nzima na sasa tunahakika kwa kupatiwa vyombo vya usafiri tutatumia saa moja, tunaishukuru serikali na tunaahidi kuwahudumia wananchi kwa kasi kubwa,"alisema Lomnyaki.

Maofisa watendaji waliopatiwa pikipiki hizo ni kutoka kata ya Bwawani Oljoro, Laroi, Musa, Oldonyowas, Oldonyosambu, Lemanyata na Sambasha.



Mratibu wa mradi wa Ketumbeine AP, uliopo chini ya Shirika la Worldvision Tanzania, Peruth Daud (wa pili kulia), akipokea zawadi ya mbuzi dume kutoka kwa Isaac Mollel wa Kijiji cha Loondoluo-Esirwa, Kata ya Gilai Merugoi, wilayani Longido mkoani Arusha juzi, baada ya kukabidhi mradi wa madarasa mawili na ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Loondolwa wenye thamani ya Sh. milioni 74.7. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Viongozi CCM walioshambuliwa waiangukia serikali

**Na Asraji Mvungi,** MONDULI

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Engaruka Juu, Wilaya ya Monduli mkoani Arusha walioshambuliwa na watu wasiojulikana wameiomba serikali kukomesha vitendo vya wananchi kujichukulia sheria mkononi vinavyoendelea kushika kasi wilayani humo.

Viongozi hao waliojeruhiwa kwa silaha za jadi ikiwamo mikuki, sime na rungu, walisema vitendo hivyo vikiendelea kupewa nafasi kuna siku itasababisha maafa makubwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwa niaba ya viongozi kwenye mkutano wa hadhara, John Laiser, alisema hivi karibuni walikumbana na kadhia ya kushambuliwa na watu wasiojulikana wakati wakisuluhisha mgogoro wa ardhi unaoendelea katika eneo hilo.

"Katika shambulio hilo baadhi ya wenzetu wamejeruhiwa sehemu mbalimbali ya miili yao. Tunaomba vitendo hivi vikomeshwe kwa kuwa ni jambo linalowezekana," alisema Laiser.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Monduli, Issak Joseph, alisema tatizo la migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo limezidi kukithiri siku hadi siku.

"Matatizo mengine yasiyokuwa ya lazima tunayalea sisi wenyewe kwa kuwa watu wakiamua kuvunja makundi ya chuki za kisiasa Monduli hakuna shida yoyote ila mambo mengi tunasababisha wenyewe na wakati umefika sasa wa kuchukua hatua," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Monduli, Wilson Lengima, alisema migogoro mingi ya ardhi inatokana na kuendekeza makundi ya kisiasa yakiwamo ya viongozi wanaoshindwa na wanaoondolewa madarakani katika uchaguzi mbalimbali kwa kuwa wamekuwa wakigeuka kuwa wapinzani unaotolewa na viongozi wapya wanaoingia madarakani.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Suleimani Mwenda, alisema atahakikisha kipindi cha uongozi wake anakomesha vitendo hivyo vya uvunjifu wa amani na alitoa onyo kwa wananchi ambao wanakubali kutumiwa na baadhi ya watu wenye maslahi binafsi.

Alisema: "Nawaomba wananchi mnipe ushirikiano nataka Engaruka iwe kata ya mfano kwa kuwa sitakubali mtu yeyote acheze maisha ya wananchi kwa kuendekeza makundi na maslahi yake, ninachowaomba mniambie ukweli."

# Wanawake jamii ya wafugaji wafanya biashara ya shanga

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WANAWAKE kutoka jamii za wafugaji wameacha kutegemea mifugo katika kuendesha maisha yao na kulazimika kufanya biashara ya shanga ili kujikwamua kiuchumi.

Hali hiyo imetokana na athari za mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha ukame wa muda mrefu na kusababisha mifugo kufa kwa kukosa maji na malisho

Wanawake hao wamekuwa wakishona na kuuza bidhaa za mikono ikiwamo shanga na viatu vya ngozi kwenye maeneo ambayo wanapita watalii katika Kijiji cha Lerang'wa Kata ya Olmolog Tarafa ya Enduiment Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha.

Mmoja wa wanawake hao, Helena Ernest, alisema wameamua kufanya biashara ya kuuza shanga kwa kuwa kutegemea mifugo pekee kumesababisha kuyumba kiuchumi baada ya mifugo yao kufa kutokana na ukame.


Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa masuala ya Uhifadhi na Utalii (KRC), Emmanuel Silayo, alisema ameanzisha kituo hicho kwa lengo la kuwezesha jamii inayomzunguka kupata kipato mbadala nje na kutegemea kilimo na mifugo.

"Niliona ni vyema nikatengeneza mazingira ya wanakijiji wa maeneo haya kupata kipato kwa kuwa kupitia wageni watakaokuwa wanakuja kutalii au wanafunzi wataweza kuinufaisha kupitia bidhaa za utamaduni watakazozalisha," alisema Silayo.

Naibu Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (MWEKA), Prof. Alex Singo, alisema kumekuwapo na tatizo la kuchelewa kuanzisha vituo kama hivyo ambavyo vinasaidia wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika.

Rais wa Taasisi ya Terre et Faune, Catherine tschanen, alisema alikutana na Emmanuel na walishauriana wawekeze kwenye kituo hicho, kitakachotumika kwa matumizi ya utafiti wa masuala ya uhifadhi na kunufaisha jamii inayozunguka.

Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Longido, Nestory Dagharo, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa kituo hicho cha utafiti na uhifadhi alisema aliyebuni wazo la kuanzisha kituo hicho hakutaka kuwa mbinafsi ili anufaike mwenyewe isipokuwa malengo yake yalikuwa ni kuwanufaisha wananchi wote.





# Mama adaiwa kumchoma moto mtoto wake kisa wizi wa karanga

**Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

MWANAFUNZI wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Bukala iliyoko Kata ya Ibisabageni (jina limefidhiwa) amechomwa moto mikono na mama yake mzazi kwa madai ya kung'oa mashina mawili ya karanga kwenye shamba la jirani yake wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Akizungumzia tukio hilo, mtoto huyo alisema siku hiyo kabla ya kung'oa karanga hizo alihisi njaa na aliamua kuingia katika shamba hilo ili apate chakula.

Alisema baada ya kuhisi njaa na ndani hapakuwa na chakula ilimbidi aende katika shamba la jirani ili aweze kung'oa karanga apate chakula. Akisimulia zaidi mtoto huyo alisema kwamba mama yake mzazi alipopewa taarifa hizo alipotoka kazini ndipo usiku alimwamsha na kumsogeza kwenye jiko la moto kisha kumchoma mikono.

Wakizungumza na Nipashe, majirani wa familia hiyo wamesikitishwa na tukio hilo na kueleza kuwa baada ya kumwona mtoto huyo ana majeraha kwenye mikono walichukua hatua na kumtafuta kiongozi wa eneo husika kwa ajili ya kupata msaada.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Bukala, Andrew Heneriko, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kuitaka jamii kuachana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, huku akichukua hatua za kumpeleka mama huyo katika Kituo cha Polisi wilayani Sengerema.

Mwenyekiti huyo alisema mama huyo amekuwa na tabia ya kwenda kazini na kuacha kiporo cha chakula au wakati mwingine hakuna chakula chochote.

Alisema mtoto huyo anapobaki nyumbani bila chakula anakuwa anahangaika bila kujua atakula wapi.

Ofisa Ustawi wa Jamii katika Kituo cha Afya Sengerema, Consolatha Magaka, aliahidi kufuatilia suala hilo ili kuhakikisha mama huyo anachukuliwa hatua ili liwe fundisho kwa wazazi wengine wenye tabia kama hiyo.

Alisema wazazi wanatakiwa kuwatimizia watoto wao mahitaji muhimu na siyo kuondoka asubuhi na kwenda kazini pasipo kuacha chakula nyumbani.



Baadhi ya mabinti wa rika balehe ambao walizaa katika umri mdogo kutoka wilayani Kishapu, Kahama na Butiama, wakiwa katika hafla ya kukabidhiwa katika vyuo vya VETA vya Kishapu, Shinyanga na Kahama juzi, kwa ajili ya kusoma bure kwa ufadhili wa Shirika la WiLDAF ili kutimiza ndoto zao. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Balozi Tanzania, Rwanda wateta namna kuwanufaisha wananchi

**Na, Titus Mwombeki,**
KAGERA

BALOZI wa Tanzania nchini Rwanda, Richard Mutayoba na Balozi wa Rwanda, Charles Karamba, wamekutana mkoani Kagera na kujadiliana namna ya kuwanufaisha wananchi fursa mbalimbali za kimaendeleo na kiuchumi zilizomo katika maeneo yao.

Akizungumza katika kikao hicho, Mutayoba alisema Tanzania na Rwanda zimekuwa na uhusiano mzuri tangu zamani na zitaendelea kudumisha ushirikiano.

Aliongeza kuwa nchi hizo kwa sasa zinashirikiana katika masuala mbalimbali yakiwamo ya usalama, biashara, elimu na afya.

Alisema hivyo ni lazima waendelee kudumisha na kushirikiana katika mambo mengine ikiwamo ya utalii, usafirishaji.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, katika kikao hicho alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara katika wilaya zilizoko mipakani ili kurahisisha shughuli za kibiashara baina ya Tanzania na nchi jirani ikiwamo Rwanda.

Gavana wa Jimbo la Mashariki la Rwanda, Gasana Emmanuel, alisema, serikali za Rwanda na Tanzania zinalenga kuboresha maisha ya wananchi wao, huku akisisitiza kuwa wananchi wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii.

## Mhagama awatangazia neema watumishi umma

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ametangaza neema kwa watumishi wa umma baada ya kuahidi kuboresha maslahi yao pamoja na kuwapandisha madaraja.

Alisema hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa baadhi yao wamekaa muda mrefu bila kupandishwa madaraja, huku akisisitiza jukumu la watumishi wa umma kutunza siri za serikali.

Mhagama alitoa kauli hiyo juzi mkoani Mwanza wakati akizungumza na watumishi wa umma alipotembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III).

Alisema kuwa serikali inaendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa umma nchini ikiwa ni pamoja na kupandisha madaraja pamoja na mishahara kwa kuwa walikaa muda mrefu bila kupandishwa madaraja.

Katika hatua nyingine Mhagama alitembelea miradi ya TASAF wilayani Ilemela mkoani Mwanza ikiwamo ujenzi wa zahanati pamoja na nyumba ya mtumishi iliyoko Mtaa wa Mihama katika Kata ya Kitangiri.

Miradi hiyo inatekelezwa kwa Sh. milioni 219 na kuitaka halmashauri hiyo kutekeleza ujenzi wa miradi hiyo ndani ya mwezi mmoja.

Aidha, aliwaagiza viongozi wa wilaya hiyo kukamilisha taratibu za kupata vikundi vya kiuchumi chini ya mradi wa TASAF vyenye sifa ili kuviwezesha kujikwamua.

Pia alitaka taratibu za kisheria zifuatwe katika kuwapata wanufaika wa miradi ya uhaulishwaji wa fedha ili pasiwe na upendeleo kwa mtu yoyote.

Mhagama pia aliutaka uongozi wa halmashauri hiyo kutoa elimu kwa wanufaika 2,880 ambao ni wanufaika wa TASAF baada ya serikali kutoa Sh. milioni 168.1 za kuinua uchumi kwa walengwa.

Alisema katika wilaya hiyo TASAF imegharamia Sh.milioni 4261 kwa ajili ya kujenga miundmbinu ya Shule ya Sekondari Nyamagana.

Akiwa wilayani Sengerema, Mhagama alipokea maombi kutoka kwa watumishi wa umma juu ya kuongezewa wafanyakazi zaidi ya 3,000 ili kuhakikisha wanaimarisha utendaji kazi katika halmashauri hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alimwahidi Waziri Mhagama kwamba atasimamia miradi yote inayotekelezwa na TASAF ili ikamilike ifikapo Machi, 28 mwaka huu.

Mratibu wa TASAF wilayani Ilemela mkoani Mwanza, Leonard Robart, alisema miradi hiyo ikikamilika itatumia Sh. milioni 219.

## Chama chaazimia 'mama kwanza', ni juhudi kuondoa ubaguzi kisiasa




Ukurasa 12

siasa

JUMATANO FEBRUARI 22, 2023

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 14

## 'BAI' MUHAMMADU BUHARI Ni Nigeria na jambo lao, wagombea mvinyo wa zamani kwenye chupa mpya

# Mwenyekiti AAFP aja na mkakati mikutano ya hadhara

## ■ Ni mkulima anayepinga chakula kuuzwa nje

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VYAMA vya siasa vinaporuhusiwa kutumia jukwaa la hadhara la kisiasa vitimize wajibu wake wa kikatiba badala ya kupindisha ajenda.

Ni angalizo kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima (AAFP), Said Soud, anayesema kazi ya vyama vya siasa ni kuielekeza serikali, kuikosoa na kuishauri hivyo mikutano ya hadhara itumiwe kutimiza majukumu hayo.

"Sisi hatufanyi majukwaa ya kisiasa kama majukwaa ya Maulidi ya kwenda kumsifu Mtume hapana. Tunakwenda kukosoana na kuelekezana maana pana tofauti kati ya mwanasiasa na shekhe," anasema Soud.

Anapozungumza na Nipashe kwenye mahojiano maalumu, anaongeza kuwa mfumo wa vyama vingi utamsaidia sana Rais Dk. Hussein Mwinyi na Dk. Samia Suluhu Hassan, kujua kasoro za watendaji na ndicho watakachokieleza katika mikutano ya hadhara ya kisiasa.

Anasema sera ya Chama cha AAFP katika mikutano ya hadhara ya kisiasa ambayo itaanza wakati wowote kuanzia sasa ni siasa ni maisha ya watu kwa sababu hali za maisha ni ngumu mno Bara na Visiwani.

Anasema watakumbusha kuwa kunahitajika kuwa na misingi imara ya uchaguzi na uadilifu ili maisha bora kwa wananchi yapatikane akitaka iwepo tafakari ya kuanzisha viwanda ili Wazanzibari wapate ajira au kujiajiri.

**MUUNDO SUKI**

Soud, anazungumzia muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUKI), akidai unaelekea umekosekana tena akidai iliyoko muundo wake haujakidhi haja.

"Muundo halali wa serikali hiyo ya umoja ripoti yake ipo hivyo ni vyema ipelekwe katika Baraza la Wawakilishi ili ikapitishwe kama sheria.

"Hatuwezi kuwa na mfumo huu chama kimoja kuingia katika serikali halafu tukaambiwa ni SUKI hii ni serikali ya mahasimu wawili...Tunahitaji muundo wa utakaokidhi hoja zetu kama taifa," anasisitiza.

**CHAKULA NI MOTO**

Soud anasema licha ya mafanikio mengi ya uongozi wa awamu ya sita, kuna mambo yanayohitaji kufanyiwa kazi ikiwamo kuzuia chakula kuvuka mipakani.

Anasema hatua hiyo ya kuzuia chakula kuuzwa nje ni muhimu kuhakikisha wananchi wanapata chakula cha kutosha kwa bei nafuu.

Anaiambia Nipashe kuwa kuruhusu vyakula kuuzwa nje kunasababisha bei kuwa juu na hali mbaya ya maisha ya Watanzania wengi.

"Serikali imefanya mambo mengi mema lakini kuna moja. Kuzuia chakula kisiende nje. Haiwezekani kiuzwe Kenya, Burundi, Congo (DR) wakati si wapigakura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ambao ughali wa chakula na mfumuko wa bei unaweza kuwa ajenda katika kampeni," anasema.

Anaongeza kuwa Watanzania wananunua kilo ya mchele hadi Sh. 3,600 na unga wa mahindi unaongezeka bei kila wakati.

Mwenyekiti wa AAFP, anaongeza: "Sasa je, Watanzania watajenga imani ya kupigakura wakati wanakabiliwa na njaa na wasiwasi wa kupata chakula?

Anakishauri chama na serikali kufunga mipaka haraka iwezekanavyo akikumbusha kuwa kuna mafanikio mengi ya kuipongeza kwa kuwatumikia vyema wananchi, lakini isisahau chakula.

"Yote mema lakini kimsingi hali ya maisha ni mbaya". Anaongeza Soud.

Aidha, anaipongeza serikali kwa jitihada za kuijenga Tanzania kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi, kuweka uwanja wa siasa za vyama vingi kwenye usawa, kuleta maridhiano na kuondoa kubaguana na ukabila, ukanda na tofauti za kidini.



Mwenyekti wa AAFP, Said Soud, akizungumzia masuala mbalimbali ya chama. PICHA: AAFP

Anasema katika miundombinu, kuna jitihada za kuboresha barabara, madaraja, bandari Bara na Visiwani na kuhakikisha Watanzania hawakwami kwenye usafiri.

Aidha, anasifu kazi ya kusambaza nishati hasa umeme mijini na vijiji ni kubwa tena kila eneo limefikiwa pamoja na kuwafikishia wananchi wengi maji safi na salama.

**KATIBA MPYA**

Said anaelezea hatua ya kuruhusu vyama kufanya mikutano ya hadhara akisema ni kuandika historia kwani hadhara hizo zitafanikisha kuibua changamoto mbalimbali zilizopo na serikali kuzifanyia kazi.

Akizungumzia kuhusu mikutano na mijadala ya katiba, anasema katiba ya mwaka 1977 ina upungufu ikihitaji kufanyiwa marekebisho lakini pia Watanzania wengi hawaifahamu.

"Kuna vuguvugu la watu kudai katiba mpya, hatuwapingi isipokuwa tunahitaji katiba iliyopo ifanyiwe kazi kwa yale ambayo hayajashughulikiwa ili itakapokuja mpya yaliyomo kwenye katiba kongwe yawe yameshafanyiwa kazi," anasema mwanasiasa huyo.

Anaitaja ibara ya 9 kifungu (i) cha katiba hiyo inayoeleza kuwa utajiri wa Tanzania utaweza kuondoa ujinga, umaskini na maradhi kwa sababu ina uwezo, ina mali zote zinazotambulika.

Anasema Tanzania ina madini ambayo ni bidhaa muhimu mfano tanzanite, gesi asilia na mafuta bidhaa muhimu kwa dunia nzima lakini ibara ya tisa ya katiba hiyo kwa Zanzibar haijafanya kazi.

"Katiba inasema itaondoa ujinga, maradhi na umaskini kwa kutumia utajiri wa nchi, nataka nikuambie kwamba serikali yetu ya Zanzibar lazima itetee ibara hiyo ili kuondoa shida hizo," anasema.

Umaskini upo na baadhi ya watu visiwani Zanzibar wanakula mlo mmoja kwa siku hivyo serikali iangalie hilo.

Anasema katiba hiyo iangaliwe na kuitendea haki Zanzibar, ikiwamo kuikwamua matatizo yaliyoainishwa katika ibara ya tisa inayoeleza kuondoa ujinga, maradhi na umaskini.

"Serikali itumikie katiba kwa sababu amekabidhiwa na 2025 imekaribia mimi kama AAFP nalitaka dola kwa hivyo nitapambana kulitafuta hivyo lazima ipambane kuweka mazingira bora kwa Wazanzibari. Watu hawashibi kwa sababu hawana uwezo wa kukidhi mahitaji yao na hasa chakula,"anasema.

**TUZO ZINAUMIZA**

Soud anazungumzia tozo, akisema Serikali ya Zanzibar imekeza kamba kwenye tozo, hivyo ni vyema kwa baadhi ya bidhaa za vyakula kuzipunguza ili kulainisha maisha ya wananchi.

Anataka serikali kuondoa tozo katika vifaa vya elimu ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi na kupata watalamu wengi.

Mwenyekiti huyo ambaye ameshashiriki uchaguzi tangu 1995 hadi 2020, anasema maisha ni magumu na yamechangiwa na uhaba wa vyakula, akiitaka SMZ kuhakikisha Wazanzibari wanapata mlo kamili kila siku.

Anatamba kuijua Zanzibar kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na baada ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 na jinsi maisha yalivyokuwa, anasisitiza kupunguza mfumuko wa bei za vyakula.




Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake wa AAFP, Shani Kitumbua (katikati), akionyesha kitabu chenye sera ya jinsia. Kulia ni Katibu wake Zawadi Nayopa na Katibu Msaidizi Magdalena Kapala. PICHA:SABATO KASIKA

# Chama chaazimia ‘mama kwanza’, ni juhudi kuondoa ubaguzi kisiasa

**Na Sabato Kasika**

MKUTANO Mkuu wa Chama cha Alliance for Africa Farmers Party (AAFP), umekubaliana kupitisha Sera ya Jinsia kwa lengo la kutaka jinsi zote ziweze kunufaika na uwepo wa vyama vya siasa.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Taifa wa chama hicho, Shani Kitumbua, anasema sera hiyo inapitishwa hivi karibuni na mkutano mkuu na kwamba sasa wanajipanga kuhamasisha umma.

Ni katika mazungumzo na gazeti hili, makao makuu ya chama hicho, Tandika Dar es Salaam, anapofafanua kwa nini wameamua kuwa na sera hiyo.

“Tumepitisha sera hii baada ya kupata mafunzo yaliyotolewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) kuhusu umuhimu wa kuwa nayo.

Wamepata mafunzo mwaka jana na kwamba wameamua kuridhia uwepo wa sera hiyo katika chama chao na kujiona kuwa walichelewa sana kuwa na sera hiyo.




Wanawake viongozi wa Chama cha AAFP wakiwa katika ofisi ya makao makuu ya chama hicho.

“Ninaamini kupitia sera hii, idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi kwenye chama chetu itaongezeka, kwa sasa tunakwenda kuhamasisha wanachama watambue umuhimu wake,” anasema Kitumbua.

Anataja baadhi ya yaliyomo katika sera hiyo kuwa ni kukuza usawa wa kijinsia na ujumuishwaji ndani ya chama, ambapo watu wote hasa wanawake na vijana na wenye mahitaji maalum watashirikishwa.

“Sera hii pia inalenga kuondoa aina zote za ubaguzi na ukatili wa kijinsia ndani ya chama, kuanzisha hatua maalum za kuhakikisha ushiriki wa makundi hayo katika utawala na utendaji, mifumo na michakato ndani ya chama,” anasema.

Mwenyekiti huyo anaongeza kuwa, sera hiyo inawezesha utekelezaji wa masuala ya jinsia ndani ya chama katika ngazi zote za utawala, lakini kuwa na mwongozo wa wazi wa afua zinazokuza usawa wa kijinsia.

“Tutaitambulisha rasmi kwa wananchi na wanachama Machi 17, mwaka huu, tutakapozindua mkutano wa hadhara jijini Dodoma ikiwa ni mara ya kwanza tangu kuondolewa zuio la mikutano ya kisiasa,” anasema.

**WADAU WAVUTIWA**

Ofisa Habari wa TGNP ambaye ni Mratibu wa Mradi wa kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi na ngazi za maamuzi, Monica John, anasema utambulisho wa sera hiyo katika vyama umeanza tangu 2021.

“TGNP ilitekeleza mradi huu unaolenga kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi wa kisiasa na ngazi za maamuzi kwa kushirikiana na WiLDAF kuanzia Novemba 2021 hadi Septemba mwaka jana,” anasema Monica.

Anafafanua kuwa, katika mradi huo, TGNP inajikita zaidi kuwajengea uwezo vyama vya siasa ili kuingiza masuala ya jinsia katika sera, mipango na miongozo yao ili kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha ushiriki mpana na wenye tija wa wanawake, katika siasa ikiwamo kuingia katika ngazi za maamuzi za vyama hivyo.

“Tanzania kuna vyama 19 vyenye usajili wa kudumu, ambapo kutokana na orodha ya viongozi wa taifa wa vyama hivyo hadi Agosti mwaka 2021, kulikuwa na wanawake wenyeviti watatu pekee sawa na asilimia 15.7.

Vyama vya CCM, SAU, huku ACT- Wazalendo kulikuwa na mwanamke anayekaimu nafasi hiyo, na kwa upande wa makatibu wakuu wanawake walikuwa ni wawili pekee sawa na asilimia 10.5 wa kutoka NCCR- Mageuzi na UDP anasema Monica.

Anasema hali bado si nzuri kwa uongozi wa ngazi za chini pia kwamba kulingana za ripoti TGNP za uwasilishi wa wanawake katika uongozi na ngazi za maamuzi Tanzania ya 2005-2020.

Anatoa mfano kwa mwaka 2019, katika ngazi ya wilaya, wenyeviti wanawake wa vyama vya siasa walikuwa ni wawili kati ya 29 ambayo ni asilimia 7 na makatibu wakuu wanawake walikuwa watano kati ya 30 ikifikia asilimia 17.

“Ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi wa kisiasa na kupunguza pengo hili la uwakilishi mdogo wa wanawake, Februari mwaka jana, TGNP iliratibu vikao vya mashauriano na vyama vya siasa, kupitia Baraza la Vyama vya Siasa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa vilivyolenga kuweka mikakati ya kuboresha mazingira ya ushindani, katika siasa ili kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye michakato ya uchaguzi,” anasema.

Aidha, anasema Juni 12 Juni mwaka jana, TGNP iliratibu kikao kingine na uongozi wa Baraza la Vyama vya Siasa, ikiwa ni mwendelezo wa vikao vya majadiliano vya kuhamasisha vyama vya siasa kuingiza masuala ya jinsia katika sera, mipango na miongozo yao, ili kuridhia masuala ya usawa wa kijinsia kuwa moja ya agenda zao za kisiasa.

Anasema kikao hicho kilifuatiwa na mkutano maalumu wa baraza Juni 13 mwaka jana ili kuweka vipaumbele vya mapendekezo yaliyotolewa na baraza hilo kupitia vikao vya mashauriano kuhusu namna bora ya kushughulikia pengo la kijinsia katika sera zao za ndani, miongozo, na taratibu.

“Pamoja na kupitisha rasimu za sera ya jinsia kwa vyama vya siasa kama hatua muhimu ya kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wanawake kushiriki katika michakato ya kisiasa na kugombea, kwa usawa katika nafasi mbalimbali za uongozi na ngazi za maamuzi,” anasema.

# Shida Afrika ni matokeo AU kuogopa kivuli chake

## •Mikataba ya ACDEG, Malabo, kufuta bunduki haijatekelezwa



Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Rais Azali Assoumani wa Comoro. PICHA: MTANDAO

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

UTAJIULIZA inakuwaje nchi yenye ardhi kubwa ya rutuba, maji mengi mabonde na mito inakuwa njaa na uhaba wa chakula usiosemeka? Tena taifa hilo halina amani na kuzidi kudumaa kimaendeleo kila mwaka? Ndiyo Afrika.

Hakuna mwenye jibu ila viongozi wa Bara la Afrika wanaijua sababu ni nini.

Wiki iliyopita wakuu wa nchi na viongozi wa serikali wa Umoja wa Afrika (AU) wanakutana jijini Addis Ababa Ethiopia, makao makuu ya Muungano wa Afrika na mambo makubwa yanayotikisa na njaa, uasi na ukosefu mkubwa wa usalama.

Wakati kikao kinafanyika, ukosefu wa amani umesambaa kwenye ukanda wote wa Sahel kwenye mataifa ya Burkina Faso, Cameroon, Chad, Gambia, Guinea, Mauritania, Mali, Niger, Nigeria na Senegal.

Hali ya usalama katika Sahel ni mbaya na vikundi vya kigaidi vinazidi kutishia maeneo ya kaskazini mwa pwani ya Afrika Magharibi.

Aidha, kukosekana utulivu wa kisiasa katika nchi kadhaa za Sahel na mivutano kati ya Mali na majirani zake umedhoofisha ushirikiano kati ya nchi tano za ukanda huo.

Mtandao wa 'Global Terrorism Index' unaeleza kuwa makundi ya 'wanajihadi' yanayofanya kazi katika nchi za Sahel ni pamoja na tawi la al-Qaeda, huko Mali ambalo pia linatishia amani Burkina Faso na Niger. Lakini, lipo Dola la Kiislamu nchini Mali. Aidha, taarifa za kuwapo kwa wanaharakati wa ISIS huko Chad nazo ni za kuhofisha.

> ACDEG imesheheni masuala mengi ya kidemokrasia, siasa safi, uongozi, uchaguzi huru na haki, uchumi na kijamii. Hata hivyo, nchi nyingi hazijahusaini mkataba na kuuridhia ikiwamo Tanzania.

MGOGORO DRC

Wakati wakuu wa mataifa ya muungano wa AU yanakutana Addis hali si shwari Congo ambalo ni taifa la pili kwa ukubwa Afrika, makundi ya wanamgambo zaidi ya 120 na vikundi vyenye silaha vinafanya kazi za uhalifu wa kivita hatari zaidi ikitoka kwa M23 inayotwaa kwa mabavu mikoa ya Goma, Kivu Kaskazini na Kivu Mashariki.

Kufikia 2008, vita vya DRC na matokeo yake vilisababisha vifo vya watu milioni 5.4, kutokana na magonjwa, njaa pamoja na vita yenyewe na kuifanya kuwa mbaya zaidi tangu Vita vya Pili. Watu wengine 1,000,000 wamekuwa wakimbizi wa ndani au waomba hifadhi nchi jirani.

UHASAMA ETHIOPIA

Taifa hili ni la tatu kwa ukubwa barani Afrika. Ni hifadhi ya wakimbizi takriban 924,000 kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) wakiwamo pia wanaotafuta hifadhi wakitokea Sudan Kusini, Somalia na Eritrea.

Kuanzia Novemba 2020, mapigano yalizuka kati ya serikali ya Ethiopia na kikosi cha waasi wa Tigray, wakiongozwa na Chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF).

Mzozo umekuwa na kusababisha vifo vya maelfu ya watu na mamilioni ya Waethiopia kuwa wakimbizi wa ndani. Takriban watu 59,000 waliikimbia Ethiopia wakipata hifadhi mashariki mwa Sudan, inasema taarifa ya mtandao wa UNHCR.

Mwaka 2011, taifa jipya la Sudan Kusini lilizaliwa ikiwa ni sherehe na shamrashamra huko Juba, ni baada ya mateso na kudhalilika kwa miongo mingi kutoka kwa Sudan ya Omar Al Bashir,

Sudan Kusini ilitarajiwa kuwa na amani na matumaini lakini miaka minane baada ya uhuru. Balaa lilizuka

Desemba 2013, mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yalizuka Juba baada ya Rais Salva Kiir kumshutumu makamu wake Dk. Riek Machar, kupanga jaribio la mapinduzi. Uasi uliendelea kati ya vikosi vya serikali vilivyo watiifu kwa kila moja.

Njaa, umaskini, vita, rushwa na uongozi usioaminiana vimeiacha Sudan Kusini kwenye fedhea kubwa na hata sasa ni eneo lisilo na amani, mbaya zaidi likizungukwa na majirani wenye vita kama DRC, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Ethiopia.

Ni viwanja vya machafuko barani Afrika vinavyoongezeka kila mwaka na kusababisha mamilioni ya raia kuteseka kwenye bara tajiri kuliko yote.

**AU INAOGOPA KIVULI**

Muungano wa Afrika una mikataba mingi ya kuleta amani, kuongeza chakula, kuachana na silaha na kudumisha haki za binadamu.

Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora ACDEG ni waraka uliopitishwa na AU Januari 30, 2007.

ACDEG imesheheni masuala mengi ya kidemokrasia, siasa safi, uongozi, uchaguzi huru na haki, uchumi na kijamii. Hata hivyo, nchi nyingi hazijahusaini mkataba na kuuridhia ikiwamo Tanzania.

Ndiyo maana nyakati za uchaguzi barani humu zimekuwa ni vilio, malalamiko, mauaji na kupinga matokeo na kuifanya Afrika kuwa nchi isiyotaka demokrasia.

**KUKOMESHA BUNDUKI**

Ni mkataba unaofahamika kama 'Silencing the Guns in Africa by 2020" Hoja ni kuondoa uasi, ugaidi na kupokonya bunduki na silaha ndogo ndogo, ili kuimarisha amani na utulivu. Afrika hilo ni jambo muhimu katika Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika, inayotaka kuwapo kwa Afrika yenye amani na utulivu wa kisiasa, kiuchumi na utangamano usio na mipaka wala pasi. Ndiyo kufikia Agenda 2063, Afrika Tunayoitamani.

Kampeni ya AU ifikapo 2020 inalenga kuwa na bara lisilo na migogoro, kuzuia mauaji ya halaiki, kuleta amani kwa wote na kuondoa vita na ukiukaji wa haki za binadamu.

Mkataba huo ni kama umebakia kwenye mashelfu kila mahali kuna vita na mauaji kuanzia DRC, Ethiopia, Afrika ya Kati na ukanda wote wa Sahel. Kwanini hakuna utekelezaji?

**KUKUZA KILIMO**

Ni Azimio la Malabo la AU lilitolewa na Wakuu wa Nchi na Serikali katika kikao cha 23 huko Malabo Equatorial Guinea, Juni 2014. Viongozi waliibuka na kaulimbiu ya 'Mwaka wa Kilimo wa Afrika na Usalama wa Chakula: "Kubadilisha Kilimo cha Afrika kwa Pamoja ...

Hadi sasa hakuna mafanikio licha ya kukubaliana kutenga fungu kubwa la bajeti kwenye kilimo asilimia 10, Afrika ina njaa.

Katika Mkutano wa Addis Ababa, masuala ya ukosefu wa amani, hali duni na machafuko ya kisiasa, umaskini, njaa na utapiamlo ndizo ajenda kuu zinazotawala, licha ya mikataba hiyo.

Mfano, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, anatangaza kutoa dola milioni 250 kutoka mfuko mkuu wa dharura (CERF) kukabili njaa na kushughulikia dharura zisizo na ufadhili wa kutosha.

Anatoa tangazo hilo kwa wanahabari jijini Addis Ababa wakati wa kikao cha viongozi wa AU, kwa mujibu wa UN NEWS.

Guterres anasema ni fedha nyingi kuwahi kutolewa na CERF na ni kutokana na ongezeko la idadi kubwa ya watu takribani milioni 339, wanaohitaji misaada ya kibinadamu na kwamba kati ya nchi wanufaika 18, mataifa 12 ni ya Afrika.

Ukiangalia Afrika kila kitu kipo kwenye mipango, mikataba na maazimio yapo ila kinachokosekana ni kuridhia mikataba wanayokubaliana na kuitekeleza. Kama AU haitasimamia mipango, maazimio, mikataba kikamilifu na kuachia kila mwanachama kuamua inavyotaka, Afrika itaendelea kuzama kwenye umaskini, migogoro ya kisiasa, njaa, vita na magonjwa licha ya kuwa ni bara tajiri zaidi duniani.

‘BAI’ MUHAMMADU BUHARI

# Ni Nigeria na jambo lao, wagombea mvinyo wa zamani kwenye chupa mpya

## •Kama Kenya Makamu Rais ‘ametoswa’, Naibu Obasanjo yumo ni Atiku Abubakar

**Na Christina Mwakangale**

KWENYE uchaguzi mkuu wa urais wapigakura milioni 93 wa Nigeria wanatarajiwa kumchagua mrithi wa Rais Muhammadu Buhari, anayemaliza muda wake kikatiba mwezi huu.

Ni mchakato wa kidemokrasia unaotarajiwa kufanyika Jumamosi wiki hii Februari 25, ukiwapeleka wapigakura kuamua ni nani wanayetaka awaongoze.

Wagombea maarufu wanaowania nafasi ya kumrithi Rais Buhari (79), ni Atiku Abubakar, wa Chama cha People’s Democratic Party (PDP) na Bola Ahmed Tinubu wa chama tawala cha All Progressives Congress.

Buhari, hatagombea tena uchaguzi amefikia kikomo cha uongozi kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo.



Rais mtarajiwa Bola Ahmed Tinubu



Muhammadu Buhari

**WANAOUTAKA URAIS**

Tinubu (70), aliliongoza Jimbo la Lagos ambalo ni mji mkuu wa kibiashara wa Nigeria kuanzia 1999 hadi 2007, amewashinda watia nia wengine 13, akiwamo Naibu wa Buhari, Makamu wa Rais Profesa Yemi Osinbajo, katika mchakato wa kura za mchujo wa chama cha APC.

Tinubu anajulikana kama ‘godfather’ wa kisiasa katika eneo la kusini-magharibi, ana ushawishi mkubwa, ingawa amekuwa akikabiliwa na madai ya rushwa kwa miaka mingi na afya mbaya, ambayo yote anakanusha.

Wengine wanasema kauli mbiu yake ya kampeni Emi Lokan, ambayo ina maana ‘ni zamu yangu’ katika lugha ya Kiyoruba, inaonyesha hali ya kustahiki.

Atiku Abubakar ni makamu wa Rais mstaafu, akiwa na miaka 76, anagombea kwa niaba ya chama kikuu cha upinzani cha People’s Democratic Party (PDP), ambacho ndicho cha Rais mstafu Olusegun Obasanjo. Amewahi kugombea kiti cha urais mara tano na zote ameshindwa.

Kwa kiwango kikubwa, kazi yake imekuwa katika ukanda wa madaraka, akiwa amefanya kazi kama mtumishi wa juu wa serikali, makamu wa rais chini ya Olusegun Obasanjo na mfanyabiashara maarufu.

Kama vile Tinubu, naye anashutumiwa kwa ufisadi na kuweka urafiki mbele jambo ambalo analikanusha.

Mwingine ni Peter Obi (61), mwenye matumaini ya kuvunja mfumo wa vyama viwili, ambavyo vimetawala Nigeria tangu mwishoni mwa utawala wa kijeshi mwaka 1999 na anagombea kwa chama kidogo kisichojulikana cha Labour.

Ingawa alikuwa katika PDP hadi mwaka jana, anaonekana kama sura mpya na anafurahia kuungwa mkono kwenye mitandao ya kijamii na vijana wa Nigeria.

Mfanyabiashara huyo tajiri amewahi kuwa gavana wa Jimbo la Anambra kusini-mashariki kuanzia mwaka 2006 hadi 2014.

Wafuasi wake, wanaojulikana kama ‘Obedients’ au watiifu wanasema ndiye mgombea pekee mwenye uadilifu, ila wakosoaji wake wanaamini kuwa kumpigia kura Obi ni kuipoteza kwa sababu hakuna uwezekano wa kushinda.

Ojei Chichi, mgombea pekee wa kike, kupitia Chama cha Allied People’s Movement (APM), kama ilivyo kwa nchi zingine za Kiafrika, hana tofauti na wagombea wengine wa kike waliomtangulia na kuonekana kiti cha urais wa Nigeria ni kwa ajili ya wanaume.

Sarah Jubril kutoka kwenye uchaguzi wa urais wa mwaka 2003, alipata kura 157,560 ambazo ndizo za juu zaidi ambazo mwanamke yeyote hajawahi kufikia hadi sasa nchini humo.

Mitazamo ya kitamaduni juu ya wanawake katika jamii mara nyingi haidumishi usawa kwa wanawake wa Kiafrika.

Uchaguzi huo, unaotarajiwa kufanyika Jumamosi wiki hii ikiwa hakuna mshindi, duru ya pili itafanyika ndani ya wiki tatu.

Pia uchaguzi huu unakwenda sambamba na wa magavana wa majimbo wenye nguvu nchini humo utakaofanyika, Jumamosi ya Machi 11, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (INEC), Mahmood Yakubu, anapuuzia mbali mapendekezo kwamba kura inaweza kucheleweshwa kwa sababu ya ukosefu wa usalama.

Nigeria, ndilo taifa lenye watu wengi zaidi barani Afrika, pamoja na utajiri wa rasilimali za kutosha yakiwamo mafuta, linakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo ukosefu wa usalama ulioenea nchi nzima.

Makundi ya waasi yameendelea kutesa nchi hiyo yenye uchumi mkubwa, tatizo kuu ni mzozo mkubwa wa kiuchumi na usawa duni unaoendelea.

Kadhalika kuna mgawanyo wa kidini na kikabila nchini humo. Kulingana na makubaliano haya ya kimya kimya, ni kwamba uchaguzi wa urais lazima ubadilishe kila mihula miwili kati ya mgombea kutoka kaskazini, awe Muislamu au kusini, Mkristo.

Lengo la makubaliano hayo ya siri, ni kudumisha uwiano katika nchi yenye makabila zaidi ya 250 tena kuliko na mivutano kati ya jamii za wenyewe kwa wenyewe.

Rais Buhari anayemaliza muda wake, anatoka kaskazini, nafasi ya urais inapaswa kuendeshwa na mgombea kutoka kusini, sasa. Ingawa PDP iliamua kupuuza kugawa maeneo kwa kumteua Abubakar, anayetoka kaskazini mashariki.

Chama tawala APC, kinatoa tiketi kwa Tinubu, anayetoka kusini, alichaguliwa mgombea mwenza.

**KAMPENI LALA SALAMA**

Mwezi Februari wakati kampeni zikielekea ukingoni joto liliongezeka, huku matusi na shutuma zikipamba moto baina ya wagombea hao wa kiti cha urais.

Mwishoni mwa Septemba mwaka jana, Serikali ya Nigeria, ilitangaza kuanza kwa kinyang’anyiro cha uchaguzi wa urais. Wagombea 18 waliingia kwenye mitano ya kampeni ya kuonyesha nia ya kuchukua uongozi.

Kampeni za kichafuana miongoni mwa wagombea zilitamba hivi karibuni, hasa wiki iliyopita, huku baadhi wakikashifiana kuhusu afya, za wagombea urais ambalo ni suala nyeti nchini Nigeria.

Inakumbukwa Rais Buhari alizua gumzo kubwa kwa kutokuonekana ikulu kwa miezi kadhaa wakati wa muhula wake wa kwanza akitibiwa nchini Uingereza maradhi yasiyojulikana.


Mwenyekiti wa Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (INEC), Mahmood Yakubu, anawahakikishia Wa- Nigeria wiki iliyopita kwamba, uchaguzi utafanyika kama ilivyopangwa Jamamosi Februari 25.

Mkuu wa tume huyo, anasema vituo 240 vya kupigia kura havitatumika katika uchaguzi huo, kwa kuwa hakuna aliyevichagua kutokana na ukosefu wa usalama katika maeneo hayo.

Vurugu za watu wanaojitenga na magenge ndio wasiwasi mkubwa kwa Wanigeria wanapopiga kura Februari 25, kwa ajili ya wabunge wapya na mrithi wa Rais Buhari.

Wapigakura wapya wanapojiandikisha nchini Nigeria, wanaruhusiwa kuchagua kituo cha kupigia kura. Watu wengi huchagua eneo la karibu zaidi na wanapoishi kwa sababu idara za usalama hupunguza harakati za usafiri siku ya uchaguzi.

*Chanzo: BBC, RFI, VOA, DW*



Makamu wa Rais aliyetoswa, Profesa Yemi Osinbajo. PICHA ZOTE: REUTERS.



‘Dada’ Ojei Chichi





## Viongozi TCCIA wapatanishwa, wamaliza tofauti zao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIONGOZI wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Mkoa wa Dodoma wametakiwa kumaliza migogoro baina yao ili kuzitumia fursa za uwekezaji ambazo zimefunguliwa na serikali ndani na nje ya nchi.

Msuluhishi kutoka TCCIA makao makuu, Wadhini Myanze, alibainisha hayo jana katika kikao cha kutatua mgogoro wa viongozi wa mkoani hapo.

Alisema mgogoro huo ulianza mwaka 2021 baada ya kufanyika kwa uchaguzi hali ambayo imekuwa ikizuia ufanisi wa chemba hiyo.

"Katika kipindi chote hicho viongozi wamekuwa na migogoro ambayo inapunguza ufanisi wa chemba hii lakini leo hii kupitia kikao hichi tumehitimisha mgogoro huu ambao uliiweka chemba katika hali ngumu kwa fursa ambazo zipo,"alisema.

Aidha, alisema mgogoro huo ulikuwa ni baina ya Mwenyekiti wa Mkoa wa TCCIA na Makamu wake watatu wa viwanda, biashara na kilimo.

Alisema kutokana na mgogoro huo mambo mengi yamekwama ikiwamo kusimamia uuzaji bidhaa nje ya nchi na kushindwa kuzitumia fursa zilizopo hivi sasa.

"Pia mgogoro huu unakosesha serikali kusikia changamoto za wafanyabiashara, wenye viwanda na kilimo ili kuzifanyia kazi hivyo tumeagiza kamati tendaji kukutana ndani ya wiki mbili ili kuweka mambo yao sawa na kama tutaona bado hawako pamoja ndani ya miezi mitatu itabidi tuitishe mkutano wa uchaguzi,"alisema.

Hivyo, aliuagiza uongozi huo kuwajibika kwa wanachama wake na kujitambulisha kwa serikali ili kushiriki jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan za kufungua milango ya uwekezaji na mataifa mbalimbali.

Mwenyekiti wa TCCIA mkoani humo, Khamis Fungameza, alisema wameyapokea maagizo hayo na wanakwenda kuyafanyia kazi.

"Naomba niwahakikishie wanachama wetu kuwa mgogoro huu umekwisha na kuanzia sasa tunakwenda kufanya kazi kama timu ili kuzitumia fursa zilizoko hivi sasa na kuisaidia serikali yetu kutafuta fursa za uwekezaji katika kilimo, biashara na viwanda,"alisema.

Alisema kutokana na Dodoma kuwa makao makuu zipo fursa nyingi ambazo wao kama TCCIA wanapaswa kuwa wa kwanza kuzifikia na kuzifikisha kwa wanachama wao ili kunufaika nazo.

# Washauri Bima ya Afya kwa Wote itumie uzoefu wa iCHF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa afya wameshauri mpango wa bima ya afya kwa wote ni muhimu utumie uzoefu wa utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) ili kuwafikia wananchi wote hususani waliopo vijijini.

Aidha, matokeo ya tathmini ya mfuko huo kwa mwaka 2022, yameonesha ni himilivu na kiwango cha michango ya wanachama kitaongezeka.

Mratibu wa CHF kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Silvery Maganza, aliyasema hayo jana jijini hapo kwenye kikao cha waganga wakuu wa mikoa na wilaya alipokuwa akiwasilisha utekelezaji wa mfuko huo kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi Desemba, 2022.

Alisema katika tathmini hiyo iliyofanywa na wataalamu kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Taifa Bima ya Afya (NHIF) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kiwango hicho kitaendelea kuongezeka hadi kufikia Sh.trilioni 1.65 mwaka 2040.

Aidha, alisema matumizi ya mfuko yataongezeka hadi kufikia Sh. trilioni 2.01 mwaka 2040.

"Uchambuzi wa ulinganifu wa mapato na matumizi ya CHF unaonesha kuwa mfuko utakuwa himilivu na hivyo kujiendesha na kutoa huduma kwa wanufaika kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi 2032 bila kutumia ziada ya mfuko,"alisema.

Alisema mfuko huo unatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 hadi 2025 na ni mpango wa bima ya afya ambao ulianzishwa ili kutoa huduma kwa wananchi walio katika ajira isiyo rasmi vijijini na mijini.

Alisema mfuko umelipa asilimia 75 ya makusanyo yake vituo vilivyotibu wanachama na kutuma, ambapo kati ya Sh. bilioni 30.167 zilizokusanywa, Sh.bilioni 22.2 zimelipwa vituoni.

Awali Mratibu wa CHF Mkoa wa Dodoma, Francis Lutalala, alisema wananchi wanawezeshwa kupata huduma za afya kwa gharama nafuu kupitia mfuko huo na wanachama 403,656 wamesajiliwa.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na Mbunge wa Viti Maalum, Fatma Toufiq, akimwongoza mwanafunzi wa Shule ya Msingi Maalum ya Buigiri, baada ya kukabidhi msaada wa fimbo za wasioona pamoja na vifaa vingine, Chamwino, mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TARURA kujenga kilomita 483 za barabara Dodoma

**Na Peter Mkwavila,**

DODOMA

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Dodoma umesema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24 umejipanga kutengeneza kilomita 483.4 za barabara zilizoko katika mkoa huo.

Matengenezo hayo ni kwa kiwango cha lami, kuzitengeneza kwa kiwango cha kokoto na ukarabati zilizoharibika.

Mhandisi wa TARURA mkoani humo, Lusako Kilembe, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza kwenye mkutano maalum wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Alisema bado kuna kilomita 699 sawa na asilimia 60 ambazo hazitaguswa kwenye bajeti hiyo ya mwaka 2023/24.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, aliutaka uongozi wa TARURA Wilaya ya Dodoma, kujikita zaidi katika kutengeneza kilometa chache za barabara kwa ukamilifu kuliko kufanya matengenezo kwa ukubwa wakati mvua zinaponyesha zinaharibu.

Alisema kuwa matengenezo ya barabara hizo chache zikitengenezwa zitaimarika zaidi kuliko zinazotengenezwa za kilometa nyingi kwa gharama kubwa.

Mavunde aalisema kuwa Jiji la Dodoma linaongoza kwa kuwa na mtandao mrefu wa barabara upatao kilometa 194.8 ikifuatia na Manispaa ya Kinondoni yenye barabara zenye urefu wa kilometa 177.





# Serikali yaandaa mpango maalum upangaji makazi vijijini

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SERIKALI kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeandaa mpango maalumu wa upangaji wa makazi ya wananchi vijijini kwa lengo la kuwasaidia wananchi kuwa na makazi bora na kuondoa migogoro.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Anjelina Mabula, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipozungumza na wataalamu kutoka katika taasisi mbalimbali zilizoko chini ya wizara yake pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali kuhusu mkakati huo.

Viongozi wengine walioshiriki kwenye mkutano huo ni wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, wenyeviti wa halmashauri pamoja na madiwani wa Jiji la Mbeya.

Alisema mpango huo unalenga kuwashirikisha wananchi, wataalamu pamoja na wadau mbalimbali wa ujenzi ili kuhakikisha vijiji vyote nchini vinakuwa na mpangilio mzuri wa makazi.

"Tumeandaa mpango huu ambao upo kwa lugha rahisi sana na unalenga kuwashirikisha wananchi kwenye upangaji wa makazi pamoja na ujenzi wa nyumba bora za makazi kwa bei nafuu," alisema Dk. Mabula.

Alisema kwa mujibu wa utaratibu ni kwamba upangaji wa makazi unatakiwa kuwashirikisha wananchi ili kuondoa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Hata hivyo alisema kwenye mpango huo kipo kipengele kinachotoa maelekezo kwa wakurugenzi wa halmashauri kuhusu hatua wanazotakiwa kuzichukua dhidi ya wanaosababisha migogoro ya ardhi.

Katika hatua nyingine Dk. Mabula alisema serikali imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 2.4 ambazo ni michango ya wananchi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya urasimishaji wa ardhi na makazi kwenye vijiji.

Alisema katika kipindi cha Julai mpaka Novemba mwaka jana mitaa 1,985 kati ya 3,397 ilirasimishwa sawa na asilimia 57.7 katika halmashauri 184 mikoa 26 Tanzania Bara.

"Kati ya mitaa hiyo 1,436 sawa na asilimia 42.3 imebainika haina miradi yoyote ya urasimishaji wa makazi na viwanja 136,291 vilipangwa na kurasimishwa kupitia michoro 948 na viwanja 89,027 upimaji wake umekamilika," alisema Mabula.

Mabula alisema katika jitihada za wizara kukabiliana na tatizo la ongezeko la makazi holela kupitia Mradi wa Kuboresha Miliki za Ardhi (LTIP) inatarajia kurasimisha mitaa 559 katika halmashauri 34 za mikoa 15 nchini.

Kamishna wa Ardhi kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mathew Nhonge, alisema kuwa bado wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kujua umuhimu wa kuwa na hati miliki pamoja na kujenga makazi kwa vibali kwa lengo la kudhibiti makazi holela na migogoro ya ardhi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon, alisema kuwa asilimia kubwa ya migogoro inayoripotiwa ni masuala ya ardhi.

"Tunapokea kesi nyingi za migogoro inayotokana na masuala ya ardhi hivyo uwepo wa urasimishaji kutasaidia kupunguza tatizo hilo kwa kuhakikisha wananchi wanajua umuhimu wa kuwa na hati miliki," alisema Mayeka.

Meya wa Jiji la Mbeya, Dor-Mohamed Issa, alisema kuwa serikali imefikisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika kuhakikisha Mbeya ya kisasa inajengwa.

Alisema wanatarajia kuzindua kampeni ya urasimishaji wa makazi katika maeneo mbalimbali ndani ya Jiji hilo ili wananchi wajue umuhimu wa kazi hiyo.




Mshindi wa promosheni ya Pilsner Lager ya kampuni ya bia ya Serengeti Breweries Ltd (SBL), ijulikanayo kama 'Kapu la Wana' kutoka Kanda ya Kusini, Justine Mwaipaja, akionesha zawadi ya televisheni aliyoshinda baada ya kukabidhiwa jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Msiwatenge waraibu dawa za kulevya, watieni moyo'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JAMII imetakiwa kutowatenga waraibu wa dawa za kulevya na badala yake iwatie moyo na kuwaelimisha ili waliotayari kuacha matumizi ya dawa hizo waache na washiriki kwenye ujenzi wa taifa.

Mtaalamu wa Saikolojia wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya Kliniki ya waraibu wa dawa za kulevya, Betuna Mwamboneke, alitoa ushauri huo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu matibabu ya waraibu hao.

Alisema jamii inatakiwa kuendelea kuwatia moyo na kuwahimiza waraibu wa dawa hizo ambao wanaendelea na matibabu kwenye vituo mbalimbali ili wasiondoke kwenye tiba hizo.

Mwamboneke alisema jamii imekuwa ikiwanyanyapaa waraibu wa dawa za kulenya, hivyo kuwafanya waendelee kutumia dawa hizo na hata wanaohitaji msaada wa matibabu ya kuachana na dawa hizo wanakosa kungwa mkono.

Alisema hali hiyo inatokana na waraibu wengi kujihusisha na vitendo vya uhalifu ikiwamo wizi na ubakaji hali iliyosababisha jamii kudhani kundi hilo halina faida yoyote.

Alisema malezi yana mchango mkubwa kwa jamii, hivyo wazazi na walezi wanapaswa kuanza kutoa elimu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto wao kwa maelezo kuwa baadhi ya wathirika wameanza matumizi ya dawa hizo wakiwa katika umri mdogo.

Alieleza sababu za vijana wengi kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya kuwa ni pamoja na ugumu wa maisha, kutaka kupunguza maumivu, migogoro ya ndoa na familia, malezi yasiyo bora, matatizo ya kimwili pamoja na upatikanaji wa dawa hizo.

Aliongeza kuwa elimu inapaswa kutolewa kwa vyombo vya usalama kujua umuhimu wa matibabu ya kisaikolojia kwa waathirika hao ili kuwasaidia kupata matibabu hata wanapokuwa wanatumikia adhabu mbalimbali.

# Wataalamu ujenzi waiangukia serikali kuhusu ajira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATAALAMU wa ubunifu na ukadiriaji wa ujenzi wameiomba serikali kuwapatia ajira kwa kuwatumia kwenye miradhi ya ujenzi wa majengo mbalimbali badala ya kuwatumia wataalamu wake wa ndani pekee.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Msajili wa Bodi ya Wabunifu na Wakadiriaji wa Ujenzi, Edwin Nnunduma, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa ubunifu na ukadiriaji majengo yaliyofanyika jijini Mbeya.

Alisema kwa sasa serikali inatekeleza miradi mingi kwa kutumia mafundi wa mitaani na hivyo kusababisha wataalamu hao kukosa ajira ambazo zingewasaidia kujipatia kipato.

"Wale wanaopewa fedha za miradi hawatumii wataalamu, kwa sababu force account imegawanyika katika maeneo mengi wanatumia hiyo sababu ya kwamba wanafanya wenyewe bila kutumia wataalamu kwa hiyo wataalamu wetu wanakosa kazi," alisema Nnunduma.

Alisema mfumo huo wa kutumia mafundi wa mitaani huwa hautumii wataalamu kwenye utekelezeji wa miradi jambo ambalo linawatia wasiwasi kwenye uimara wa miradi. Hivyo aliwaomba wananchi wanaotaka kujenga nyumba ama majengo ya aina yoyote kuwatumia wataalamu hao ili majengo yao yadumu kwa muda mrefu bila kuharibika.

Kadhalika, aliiomba serikali kuharakisha utugwaji wa sheria ya ujenzi itakayosaidia kudhibiti ujenzi holela katika maeneo mengi ambao unasababisha madhara mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Alisema kwenye sekta ya ujenzi kuna sheria ambazo zinatakiwa zitumike kwenye usimamizi wa ujenzi ili kuhakikisha makazi na taasisi mbalimbali ili kuwe na mpangilio mzuri wa miji.

Alisema mbali ya kuwajengea uwezo wataalamu hao kuhusiana na masuala ya kitaaluma pia bodi hiyo imewapa mafunzo kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa serikali kutokana na kazi wanazofanya kwa maelezo kuwa ni wajibu wa kila Mtanzania kulipa kodi. Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, ambaye alikuwa mgeni rasmi alishauri wataalamu hao kutembelea maeneo ya wilayani na kwenye halmashauri ambako ndiko kuna miradi mingi kuliko kuendelea kukaa maeneo ya mjini.

Alisema wakati mwingine wataalamu hao hawashirikishwi kwenye miradi kwa sababu huwa hawajitambulishi na hivyo kutojulikana kabisa kwa viongozi.

Pia alitoa rai kwa vijana wanaohitimu katika fani za ubunifu na ukadiriaji wa ujenzi kujiajiri baada ya kuhitimu kwa kujiunga kwenye vikundi na kubuni miradi mbalimbali ya kimaendeleo na kisha kuomba mikopo kwenye halmashauri kwa ajili ya kuendesha miradi hiyo.

Baadhi ya wadau walioshiriki kwenye mafunzo hayo waliwataka wabunifu na wakadiriaji wa majengo kuhakikisha wanasaidia kuwaelimisha wananchi kuhusu kujenga majengo kwa kutumia vifaa vyenye ubora.

Mwakilishi wa Taasisi ya Dar Ceramic Center Kanda ya Mbeya, John Gondwe, alisema wateja wengi hawajui matumizi ya vifaa bora kwa ajili ya ujenzi, hivyo wanahitaji elimu ili kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa na matumizi ya vifaa hafifu.



# Rais Mwinyi azitaka taasisi za dini kuhubiri amani, maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema taasisi za dini na za kiraia zina mchango mkubwa kwa serikali hasa kwenye jukumu la kuendeleza amani na maendeleo nchini.

Alisema taasisi za dini zina jukumu la kutoa huduma za kiroho, zinasaidia kujenga taifa lenye amani, mshikamano na maadili kwa jamii jambo linaloimarisha amani na maendeleo.

Aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Askofu Mkuu wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, Jimbo Kuu la Kusini mwa Tanzania, Dk. Godwin Lekundayo aliyefika na uongozi wake kujitambulisha.

Alisema taasisi hizo zinaushirikiano mzuri na serikali katika ustawi wa jamii bora na kustawisha mshikamano wa imani na kiroho katika kukuza vijana waadilifu.

"Amani utulivu, umoja na maridhiano ni mambo ya msingi katika nchi yoyote na kuongeza kuwa amani inapokosekana mambo mengi hushindikana kutekelezwa kwa wakati unaostahiki yakiwamo maendeleo hata uhuru wa kufanya ibada," alisema.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi aliwapongeza viongozi hao kwa kuendelea kuhubiri na kuhamasisha amani kwa imani zao na kueleza licha ya taifa kuwa na mchanganyiko wa waumini wenye imani tofauti lakini linasonga mbele kimaendeleo. Hata hivyo, alizitaka taasisi hizo za dini kuendelea kuisaidia serikali kulea taifa lenye uadilifu na vijana watiifu ili kujenga taifa lenye viongozi bora.

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Sabato Tanzania, Dk. Godwin Lekundayo, alisifu juhudi za maendeleo zinazofanywa na Serikali ya Zanzibar kwa hatua iliyopiga ndani ya kipindi cha muda mfupi na kuzipongeza serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar kwa kuimarisha umoja na mshikamano bila kujali tofauti za imani za wananchi.

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Mwinyi alishiriki halfa ya ufunguzi wa ubalozi mdogo wa Umoja wa Nchi ya Falme za Kiarabu (UAE), Zanzibar ambapo Balozi Mdogo wa Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Saleh Al Hemeir, aliwakaribisha wananchi wa Zanzibar kwenye ofisi hizo kuhudumiwa masuala mbalimbali ya kidiplomasia.



Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Bakari Hamad (katikati), akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa mjini Zanzibar jana, kuhusu mikutano ya hadhara ya vyama hivyo inayotarajiwa kuanza hivi karibuni. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wananchi Zanzibar wahimizwa kushiriki ulinzi shirikishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imewataka wananchi kujitokeza kushiriki katika ulinzi shirikishi katika jamii ambao kwa kiasi kikubwa utasaidia kupambana na matukio ya uhalifu yanayojitokeza na kuleta hofu kwa wananchi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la mwakilishi wa viti maalumu wanawake, Salha Mohamed Mwinjuma, akiyetaka kujua mikakati inayochukuliwa na serikali katika kukabiliana na uhalifu.

Waziri Juma alisema miongoni mwa mikakati inayochukuliwa na serikali kwa sasa ni kuwataka wananchi kuanzisha ulinzi shirikishi katika maeneo wanayoishi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Alisema Jeshi la Polisi lipo kwa mujibu wa sheria katika kuweka ulinzi wa amani na mali za wananchi kuwa salama na matukio ya uhalifu.

Aidha, aliwataka wazazi kuhakikisha wanafuatilia mwenendo na tabia za vijana wao ambao ndiyo wanaojishughulisha na matukio ya vitendo vya uhalifu katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

Alisema matukio ya uhalifu yanayofanyika katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba ikiwamo ya kutumia silaha za jadi yanafanywa na wananchi wa Zanzibar.

# 'Makamanda Jeshi la Polisi simamieni sheria wakati wa mikutano ya hadhara'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamadi Bakari Hamad, amewataka makamanda wa mikoa wa jeshi hilo Zanzibar, kwenda kusimamia sheria wakati wa mikutano ya hadhara.

Alisema askari polisi wasiende katika mikutano ya hadhara kama washabiki wa vyama bali waende kama wasimamizi wa sheria ambapo jukumu lao ni kuhakikisha ulinzi unaimarika kipindi chote kabla na baada ya mikutano.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa kuhusu mikutano ya hadhara ambayo inaanza hivi karibuni.

Alisema Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na nguzo muhimu ni utawala wa sheria ambao huwafanya watu watambue mipaka ya mahusiano kati yao na vyombo vya dola na vyama vya siasa.

Hamad alisema kukiwa na uelewa wa pamoja juu ya nguzo muhimu ya demokrasia ni rahisi kujiepusha na mivutano na migogoro isiyo ya lazima kwa sababu kila mmoja atajua hatima ya mambo anayoyapanga kuyafanya. Alisema mikutano huanza na maandalizi hivyo aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuwa wanafursa ya kujipanga ya kuepusha migogoro isiyo ya lazima miongoni mwa vyama vyenyewe na pia baina ya vyama na Jeshi la Polisi.

Kamanda Hamad alisema vyama vya siasa vinahaki ya kuufahamisha umma mitazamo tofauti ya vyama vyao na vile vyama ambavyo havijapata fursa ya kuunda serikali vinawajibu wa kuikosoa serikali.

Alisema katika kutumia haki hiyo vyama hivyo vinawajibu wa kuhakikisha ukosoaji unafanyika kwa namna isiyochochea vurugu na machafuko, bila ya kutumia lugha za kichochezi, matusi na kushambulia faragha na maisha ya watu binafsi.

Kamanda Hamad alisema wito wake ni ukosoaji miongoni mwa vyama na baina ya vyama na serikali ufanyike kwa kuzingatia uzalendo na kuheshimu mila, desturi na maadili ya nchi.

Alisema Jeshi la Polisi wajibu wao ni kusimamia utekelezaji wa sheria ikiwamo sheria zinazolinda haki za kisiasa na wanajukumu la kuimarisha usalama katika mikutano ya vyama vya kisiasa bila ya kubagua chama chochote.

Kamanda huyo alisema haimanishi kwamba wakati wa utekelezaji wa jukumu hilo wanapaswa kuwa vipofu na viziwi juu ya yale yanayoendelea katika mikutano hiyo. Aidha, alisema watakuwa makini na kusikiliza ushahidi kwa yanayotokea katika mikutano hiyo na hawatasita kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yoyote atakayetumia jukwaa la kisiasa kufanya kitendo chochote kinachochochea vurugu na uvunjifu wa amani.

Alisema wamejiandaa kwenda kusimamia mikutano ya hadhara, ifanyike kwa amani na utulivu ambapo azma hiyo itafanikiwa kwa ushirikiano baina ya vyama vya siasa na Jeshi la Polisi.

Alisema vyama vya siasa vinapaswa kutoa taarifa ya mikutano yao saa 48 kabla ya mikutano hiyo ili Jeshi la Polisi kupata fursa ya kujipanga ya kuwapatia ulinzi katika mikutano hiyo.

Mkuu wa Utawala Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Saleh Mohammed Saleh, alisema ulinzi na usalama wa raia na mali zao ni miongoni mwa majukumu matano makubwa waliyokabidhiwa.

Alisema jeshi hilo linakusudia kufanya vikao kama hivyo viwe endelevu kwa lengo la kujenga imani kati yao na raia hasa kipindi hiki ambacho dunia imeingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya kisiasa.

Wakitoa maoni yao, viongozi wa vyama vya siasa waliohudhuria kikao hicho walisema Zanzibar inaweza kwenda vizuri kwa amani iwapo vyombo vya ulinzi hasa Jeshi la Polisi havitakubali kuingiza utashi wa kisiasa katika kutekeleza majukumu yao.

Hivyo walilishauri jeshi hilo kujitathmini kikamilifu ili kuwabaini baadhi ya watendaji wake wanaokiuka maadili katika kazi kwa kile walichodai kulipa fadhila baada ya kupata ajira hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KEFA YONAS KUPA**, Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK II** yenye namba za usajili **T428AFV, CHASSIS NAMBA 150105130, ENGINE NAMBA 1G 5234248** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/56002/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MPWAPWA**
**KITUO CHA MPWAPWA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 5 MWAKA 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAROLD JIM MWASIGALLAH**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA MARGARET JIM MWASIGALLAH**

### TANGAZO

**(Kanuni namba 75 ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Gazeti la Serikali Na. 369 Mwaka 1963)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 9 Mwezi wa 3 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamiz wa mirathi hiyo.
**Zingatia:** Endapo kunal yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leot tarehe 16 Mwezi Februari Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI
RESIDENT MAGISTRATE
MPWAPWA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......15/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: BAKARI AHMED CHADDY WA SULTAN AREA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA**
**1;MARIRO SHABAN**
**2;HAMIDA ABDALLAH**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 3 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 02 mwaka 2023

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MADAI NA. 4/2023**
**YASSIRI MOHAMED SIMBA.......... MDAI**
**DHIDI YA**
**LEONARD SHIMBA.................MDAIWA**

### WITO/KUITWA SHAURINI

**LEONARD SHIMBA**
**POPOTE ULIPO**
Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 27/02/203 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.
Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.
Imesainiwa leo tarehe 15 Mwezi 02 Mwaka 2023

E. C. LUKUMAI
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MFAWIDHI
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi na 40|2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SEFU MOHAMED SUDI**
**KATIKA SHAHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIOLETWA NA JOKHA SEFU MOHAMED**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa.
Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetotewa leo tarehe 21 Mwezi 02 mwaka 2023**

HAKIMU
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIAM ABDULNUR KASHENDWA**

Anatangaza kupotelewa kwa Kadi ya gari aina ya **FUN CARGO** Yenye namba za usajili **T 896 DQR (Chassis no NCP 200352675).** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu au piga cm no **0718779565.**
**DSM/PHQ/RB/69901/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na. 10/2023**
**ANNA JOSEPH SANGA.......................Marehemu**
**FROLA PETRO KYANDO............................Msimamizi**

### TAARIFA KWA WADAI

**(Kanuni ya 9 (1) ya Nyongeza ya V ya Sheria ya Mahakimu wa Mahakama Sura ya 11 Rejeo la 2019)**

**TAARIFA** inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu mtajwa hapo juu ANNA JOSEPH SANGA, aliyefia Makowo-Njombe tarehe 23 Juni 2022, na Mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo mimi FROLA PETRO KYANDO siku ya tarehe 15 Februari, 2023, hapa sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia namba sanduku langu la barua....... Njombe au namba ya simu............. au kuniletea kwa binafsi, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoishia nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili, nikizingatia tu madai ambayo nitakuwa nimearifiwa.

**FLORA PETRO KYANDO**

---


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## 3 wauawa tetemeko jipya Uturuki

**INSTANBUL,** UTURUKI

TETEMEKO la ardhi jipya lenye kipimo cha 6.4 limeua watu watatu na kujeruhi wengine zaidi ya 200 katika baadhi ya maeneo ya Uturuki yaliyoharibiwa wiki mbili zilizopita na tetemeko kubwa lililoua maelfu ya watu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na maofisa nchini Uturuki, tetemeko hilo lilitokea juzi jioni kwamba majengo zaidi yaliporomoka, na kuwanasa baadhi ya watu, huku kukiripotiwa idadi ya watu wengi waliojeruhiwa katika nchi jirani ya Syria.

Inaelezwa kuwa kitovu cha tetemeko la Jumatatu kilikuwa katika mji wa Defne, katika mkoa wa Uturuki wa Hatay, eneo lililoathirika vibaya katika tetemeko mwanzoni mwa mwezi huu lililokuwa na ukubwa wa kipimo cha 7.8.

Taarifa zilieleza kuwa tetemeko hilo jipya lilisikika pia nchini Syria, Jordan, Cyprus na Misri, likifuatiwa na tetemeko la pili la kipimo cha 5.8.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Uturuki, Suleyman Soylu, alisema juhudi za kuwatafuta na kuwaokoa manusura zinaendelea katika majengo matatu yaliyoporomoka, ikielezwa kuwa watu sita wakisadikiwa kuwa wamenaswa. **VOA**

## Takribani wanajeshi 51 wauawa Burkina Faso

**OUAGADOUGOU**, BURKINA FASO

RIPOTI ya awali ya makao makuu ya jeshi nchini Burkina Faso imesema wanajeshi wasiopungua 51 waliuawa katika shambulio lililotokea Februari 17, mwaka huu katika eneo la Sahel.

Mapigano makali yaliripotiwa kati ya wanajeshi wa Burkina Faso na kundi la kigaidi lenye silaha kati ya maeneo ya Oursi na Deou katika jimbo la Oudalan wiki iliyopita.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa huwenda idadi hiyo inaweza kuongezeka katika saa zijazo kwasababu wanajeshi kadhaa bado hawajulikani walipo.

Chanzo cha usalama kililiambia shirika la habari la RFI, kwamba karibu watu 80 bado wanatafutwa.

"Waliojeruhiwa wanatibiwa katika vituo vinavyofaa vya matibabu kwa ajili ya huduma na helikopta za jeshi la anga zimeanza kusafirisha miili ya wanajeshi waliouawa wakati wa shambulio hili kwenda mji mkuu Ouagadougou," kilisema.

Kwa mujibu wa maofisa wakuu wa majeshi, wanajeshi wa Burkina Faso walikuwa katika kazi yao ya kila siku waliposhambuliwa na watu wenye silaha.

"Kikosi hicho kililengwa na shambulio tata na mapigano makali yakatokea," alisema.

Hata hivyo ilibainishwa kuwa shambulio hilo lilifanyika kati ya maeneo ya Oursi na Deou, katika eneo la Sahel, karibu na mpaka wa Mali na kwamba wanajeshi wengi walitumwa kwenye eneo la tukio wikiendi nzima.

Kwa mujibu wa duru za kijeshi magaidi zaidi ya 100 waliuawa na magari kadhaa pamoja na vifaa vya kijeshi kuharibiwa, ikibainisha kuwa washambuliaji walikuwa wakijaribu kutoroka kuvuka mpaka wa kaskazini kuelekea Mali, wakati walilengwa na jeshi la anga la Burkina Faso. **RFI**

# Putin ayatupia lawama mataifa ya Magharibi

**MOSCOW,** RUSSIA



RAIS wa Russia, Vladmir Putin, amezilaumu nchi za magharibi akisema zinaendelea kumimina fedha kuunga mkono vita na kwamba nchi hizo zilianza kuifanya Ukraine kuwa mpinzani wa taifa lake muda mrefu.

Katika hotuba yake ya mwaka aliyoitoa jana nchini Russia, Rais Putin, alisema nchi hizo zinawajibika kubeba dhamana kikamilifu juu ya vita hivyo vinavyoendelea kati yake na Ukraine.

Aidha, mara kwa mara kiongozi huyo wa Russia, amekuwa akitoa sababu za kuhalalisha uvamizi wake nchini Ukraine kwa kuzituhumu nchi za Magharibi kwamba zinaitishia nchi yake.

Katika hotuba yake ya jana pia alirudia hayo hayo akisisitiza kwamba nchi za Magharibi ndizo zilizoanzisha vita hiyo na kwamba Russia inatumia nguvu kuimaliza vita hiyo na inapambana kurudisha haki ya kihistoria.

"Hatua kwa hatua tutayamaliza matatizo yanayotukabili kwa uangalifu na kwa ustadi," alisema Putin. **DW**




Mwonekano wa majengo yaliyoharibiwa na tetemeko jipya la ardhi lililotokea juzi jioni nchini Uturuki. **PICHA: DW**

# Hali tete Nigeria kuelekea uchaguzi mkuu wa urais

**ABUJA,** NIGERIA

ZIKIWA zimebaki siku chache kabla ya Nigeria kufanya uchaguzi wa Rais, maofisa watano wa polisi wameuawa katika mashambulio mawili tofauti huku waandamanaji wakichoma benki mbili kutokana na uhaba wa noti za Naira.

Zaidi ya wapigakura milioni 90 wameandikishwa kushiriki kura ya Jumamosi kumchagua mrithi wa Rais Muhammadu Buhari ambaye atakuwa anamaliza mihula miwili madarakani.

Kuelekea kura hiyo, nchi hiyo inakabiliwa na vitisho tofauti vya kiusalama ikiwa ni pamoja na chachu ya wale wanaotaka kujitenga katika eneo la kusini mashariki lakini wanamgambo wa Kiislamu wenye itikadi kali katika eneo la Kaskazini Mashariki, pamoja na magenge ya utekaji upande wa Kaskazini Magharibi.

Msemaji wa polisi Ikenga Tochukwu, alisema washukiwa wanaotaka kujitenga walivamia kituo cha polisi cha Awada juzi kwa kutumia vilipuzi na bunduki.

Aidha, polisi walisema mwishoni mwa wiki iliyopita walizuia shambulio jingine kwenye kituo cha polisi cha NkwelleEzunaka na siku moja iliyopita, washambuliaji walikuwa tayari wamevamia kituo cha polisi katika eneo la Ogidi na kuwaua polisi watatu.

Inaelezwa kuwa polisi wanalishutumu kundi lililopigwa marufuku la watu wa asili wa Biafra IPOB sambamba na tawi lake lenye silaha la mtandao wa usalama wa Mashariki ESN kwa kufanya mashambulizi ya mara kwa mara, madai ambayo wanakanusha.

Inabainishwa kwamba Jumatatu kulishuhudiwa ghasia nyingine katika jimbo la Ogun ambako waandamanaji walichoma moto benki mbili katikati mwa uhaba wa pesa taslimu za Naira.

Gazeti la Punch limenukuliwa likisema kwamba ghasia hizo zilizuka kwenye mji wa Sagamu baada ya mashine za benki za kutolea fedha ATM kushindwa kutoa pesa taslimu.

Video zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii zimeonyesha wakaazi wakishuhudia wateja waliojawa na hasira wakichoma moto benki.

Polisi wanadai kuwa wamewakamata watu 27 kuhusu matukio hayo na kwamba hali ya utulivu imerejea.

Nigeria inakabiliwa na mgogoro wa uhaba wa noti za Naira wakati serikali ikishinikiza matumizi ya noti mpya kwenye bili ambazo zimechapishwa kabla ya uchaguzi wa Jumamosi.

Samuel Oludare ni kijana anayetarajiwa kushiriki zoezi hilo na anasema kwamba "ninaamini kura yangu itakuwa na umuhimu, lakini nina hofu kunaweza kuwa na wizi wa kura unaofanywa na watu ambao wanahisi hawawezi kushinda na watafanya mbinu zote muhimu za kuvuruga uchaguzi."

Mfumuko wa bei sasa umefikia asilimia 21.8, na kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana sasa ni asilimia 43. **DW**

# AFRICAN LYON, STAND UNITED ZATESA 'FIRST LEAGUE'

**Na Adam Fungamwango**

TIMU zilizowahi kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, African Lyon na Stand United, zinaongoza 'first league', ambapo kwa mfumo wa sasa ni kama Ligi Daraja la Pili nchini.

Timu hizo zinaonekana kujipapatua ili kupanda na msimu ujao kucheza Ligi ya Championship, zamani ikiwa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Wakati African Lyon ikiongoza kwenye Kundi A, Stand United ni kinara wa Kundi B.

Katika michuano hiyo inayocheza kwa makundi mawili, African Lyon iliyoshuka daraja Ligi Kuu msimu wa 2020/21, inaongoza kwa pointi 14, lakini ikikabwa koo na timu Lipuli FC yenye pointi kama hizo, lakini Dar City pia ina idadi hiyo ya pointi.

Hata hivyo, African Lyon ipo juu kwa sababu imefunga mabao 15, Lipuli 13 na Dar City 10, huku timu zote zikiwa zimecheza mechi saba.

**Timu ya Cosmopolitan iko kwenye nafasi ya nne kwa pointi 11, TRA FC pointi nane, Tunduru Korosho nafasi ya sita, ikiwa haina pointi.**

Stand United iliyoporomoka daraja kutoka Ligi Kuu msimu wa 2018/19, inaliongoza Kundi B ikiwa na pointi 18, ikicheza mechi nane, ikifuatiwa na TMA FC, yenye pointi 17, Rhino Rangers nafasi ya tatu, pointi 16, Alliance FC iko nafasi ya nne na pointi zake 15, Kurugenzi nafasi ya tano pointi 11, Kasulu United nafasi ya sita ikiwa na pointi tano, Mwadui FC nafasi ya saba, ikiwa na pointi mbili na timu Mbao FC ikiburuza mkia ikiwa na pointi moja tu.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya wenye ulemavu wakifanya mazoezi katika Viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Bondia Kidunda kumvaa Mukala Ijumaa*

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa, Patric Mukala kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) ametua nchini jana usiku tayari kwa pambano lake la kuwania mkanda wa Ubingwa wa Afrika, ABU, katika uzani wa Super Middle dhidi ya Mtanzania, Seleman Kidunda.

Mukala ambaye atacheza pambano kuu dhidi ya Kidunda katika pambano hilo linalotarajia kupigwa Februari 24, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza.

Akizungumza na gazeti hili jana, promota wa pambano hilo kutoka Kemmon Sports Agency, Saada Salum alisema kuwa Mukala na jopo lake la ufundi wanatarajia kutua nchini usiku wa jana.

Alisema maandalizi yote yanaenda vizuri kuelekea pambano na tayari Mukala ameshatua nchini kukabiliana na mpinzani wake, Kidunda na ana imani litakuwa pambano la aina yake kwa sababu ya historia ya mabondia hao.

"Mpinzani wa Seleman Kidunda, Patric Mukala, tumempokea akitokea Afrika Kusini tayari kwa pambano lake la kuwania mkanda wa ABU dhidi ya Kidunda," alisema Saada.

Aliongeza: "Kama tulivyowaambia awali kwamba Kemmon Sports Agency tumejipanga kuleta mapinduzi katika mchezo wa ngumi hivyo tunaomba waendelee kununua tiketi katika vituo ambavyo vimekuwa vinauza ambazo zinapatikana kwa bei ya Sh. 10,000, Sh. 20,000 na Sh. 50,000 kwa VIP A," alisema Saada.

## Polisi yajipanga kuwaweka korokoroni Tanzania Prisons

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya matokeo ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Prisons, Polisi Tanzania imejinasibu kwa kusema ilijipanga kushinda mchezo huo.

Polisi ipo nafasi ya 15 ya msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa inapambana kujinusuru isishuke daraja ikiwa na pointi 19 katika mechi 23 mbele ya Ruvu Shooting inayoshikilia mkia ikiwa na pointi 17.

Juzi Polisi ilifanikiwa kuibuka na alama tatu baada ya kuwafunga Prisons, bao lililofungwa na Celvin Sabato na hivyo kuwafanya wapande hatua moja juu.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Polisi, Frenk Rukwalo, alisema kuwa wamefurahishwa kuibuka na ushindi japo mchezo ulikuwa mgumu.

"Goli la Sabato limetusaidia kupata alama tatu, niseme tu tangu awali nilisema kwamba mchezo huu utakuwa mgumu," alisema Rukwalo.

"Kama ilivyo ada tulisema tungeibuka na ushindi na kweli hilo limefanikiwa nitoe pongezi kwa wachezaji wetu na tunajipanga kufanya vizuri michezo inayofuata," aliongeza.

## Soka la ufukweni kusaka vipaji Kigoma, Mwanza

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni, Boniface Pawassa, amesema ana programu maalumu ya kusaka nyota katika mikoa ya Kigoma na Mwanza kwa lengo la kukuza mchezo huo.

Hivi karibuni kocha huyo alikuwa Mtwara pamoja na benchi la ufundi kwenye mashindano ya Majeshi ambapo amefanikiwa kupata wachezaji 10.

Akizungumza na Nipashe, Pawassa alisema kuwa kuna mikakati waliyoiandaa ya programu maalumu ya kusaka vipaji nchi nzima ambapo wataanzia katika mikoa ya Kigoma na Mwanza.

"Tunahitaji kuuendeleza mchezo huu nchi nzima ili mchezo uweze kutambulika, tuna programu nyingi na tumechagua Kanda ya Magharibi na tutaanza na Kigoma kisha Mwanza.

"Lengo la kwenda huko ni kuanzisha mchezo wa soka la ufukweni ambapo programu hiyo itafanyika mwezi wa nne ambapo benchi lote la ufundi litakuwa huko ikiwa ni pamoja na kuangalia wachezaji.

"Aidha, tukimalizana na tour ya Kanda ya Kaskazini tutaelekea upande wa Mtwara na Lindi kuanzisha mchezo huo na kuangalia wachezaji pia," alisema Pawassa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**FATI HAITAKI MAN**
MSHAMBULIAJI wa Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 20 amekuwa akihusishwa na Manchester United, lakini amesema ana mkataba na Barcelona hadi 2027 na anatumaini kusalia na klabu hiyo ya LaLiga kwa miaka mingi zaidi. (***Mirror***)

**THURAM AGOMBEWA**
ARSENAL, Chelsea na Manchester United zote zinavutiwa na mshambuliaji wa Ufaransa, Marcus Thuram mwenye umri wa miaka 25 ambaye atakuwa mchezaji huru msimu huu wa joto baada ya kukataa mkataba mpya na Borussia Monchengladbach. (Talksport)

**TUCHEL KURUDI PSG**
KLABU ya Paris St-Germain inajiandaa kumteua tena kocha wa zamani wa Chelsea, Thomas Tuchel kama kocha wa klabu hiyo, baada ya kumtimua Mjerumani huyo mnamo Desemba 2020. Christophe Galtier kwa sasa ndiye kocha wa kikosi hicho cha Ligue 1. (***Evening Standard***)

**MCTOMINAY KUUZWA**
KLABU ya Manchester United iko tayari kusikiliza ofa kwa kiungo wa Scotland, Scott McTominay na wanaamini wanaweza kupata pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Football Insider***)

**GARNACHO SAFI MAN**
KLABU ya Manchester United imekubaliana kimsingi na mshambuliaji wa Argentina mwenye umri wa miaka 18, Alejandro Garnacho juu ya mkataba mpya wa miaka mitano. (***ESPN***)

**MOYES KUTIMULIWA**
KOCHA wa West Ham, David Moyes anatazamiwa kutimuliwa ikiwa timu yake, ambayo iko katika eneo la kushushwa daraja Ligi Kuu ya England, itapoteza nyumbani dhidi ya Nottingham Forest Jumamosi. (***Mirror***)

**GRACIA ATAJWA LEEDS**
KLABU ya Leeds United iko kwenye mazungumzo na kocha wa zamani wa Watford, Javi Gracia kuhusu nafasi ya ukocha iliyo wazi katika klabu hiyo. (***Guardian***)

**SPURS HAKIELEWEKI**
MMILIKI wa Tottenham Hotspur, Joe Lewis na mwenyekiti Daniel Levy hawana uhakika iwapo watasikiliza ofa kwa klabu nzima, kuuza hisa ndogo au kusalia katika udhibiti wa klabu. (***Evening Standard***)

**BAJCETIC NA LIVERPOOL**
BABA wa kiungo wa kati wa Liverpool na Hispania, Stefan Bajcetic mwenye umri wa miaka 18 amesema Wekundu hao wasingemsajili mwanawe kutoka akademi ya Celta Vigo hadi walipojua kwamba wapinzani wao Manchester United wanamtaka. (***El Mundo, via Sport Witness)***

**SANTOS KWA MKOPO**
CHELSEA ipo kwenye mazungumzo na mshambuliaji wa Brazil, Andrey Santos ili kumpeleka kwa mkopo Palmeiras baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kunyimwa kibali cha kufanya kazi. (***Evening Standard).***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MODRIC ATOA YA MOYONI MKATABA MPYA MADRID

### Asema ikiwa hataweza kutoa mchango mkubwa atakuwa tayati kuondoka na...

**MADRID,** Hispania

LUKA Modric hajafanya mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na Real Madrid na aliapa anataka kubakia katika klabu hiyo.

Mkataba wa nahodha huyo wa Croatia pale Madrid unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, lakini anatamani kubaki na mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Klabu Bingwa ya Dunia.

Kiungo Modric alifichua wakati wa kuelekea mchezo wao wa jana Jumanne hatua ya 16 bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool kuwa hakuna maendeleo yoyote kuhusu mustakabali wake.

Mchezaji huyo wa muda mrefu mwenye umri wa miaka 37 alisema kwamba hatabaki Santiago Bernabeu ikiwa anahisi kuwa hataweza kutoa mchango mkubwa.

Alisema: "Siwezi kusema lolote kuhusu mkataba mpya kwa sababu sijazungumza na klabu, nimetulia sana, huwa narudia yale yale, nataka kuendelea hapa, najisikia vizuri na nataka kuendelea kucheza Madrid. "Lazima nizungumze na kujua klabu inachofikiria. Nataka kustahili kuendelea, sio kupewa mkataba mpya kama zawadi. Hakuna mtu aliyewahi kunipa chochote. Nataka kuendelea bila sifa.

"Hakuna kinachoweza kubadilisha uhusiano wangu au mawazo yangu na klabu. Madrid ni klabu ya maisha yangu na hakuna mtu anayeweza kuivunja au kuibadilisha.

"Nimekuwa hapa kwa miaka 11 na najua mahitaji ni ya juu zaidi. Mambo mengi yanasemwa kutoka nje, ni kawaida kwa sababu ni klabu bora zaidi duniani. Toni (Kroos) na mimi tulicheza pamoja kabla ya Kombe la Dunia na sasa inaonekana kwamba hatuwezi.

"Tumeshinda sana. Hainisumbui, nimeshazoea. Lazima tufanye vizuri."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,080,3

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# OSIMHEN: NAWEZA KUONDOKA NAPOLI

**NAPLES,** Italia

IMERIPOTIWA kuwa mchezaji anayelengwa na Manchester United na Chelsea, Victor Osimhen amekataa kuondoa uwezekano wa kuhama katika dirisha lijalo la usajili, ingawa nyota huyo wa Napoli analenga kutwaa taji kwanza.

Osimhen amefunga mabao 18 kusaidia Napoli kuongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa tofauti ya pointi 15 - Erling Haaland wa Manchester City ndio pekee (26) aliyemzidi kwa mabao mengi katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria alifunga katika mechi ya saba mfululizo ya ligi wakati Napoli ilipoichapa Sassuolo mabao 3-0 wiki iliyopita, na kiwango chake cha kuvutia kimeripotiwa kuwavutia miamba wa Ligi Kuu ya England.

United na Chelsea zote zimetajwa kumtaka Osimhen, ambaye rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis amesisitiza hauzwi.

Huku akionekana kuelekea kuwasaidia Partenopei hao kutwaa Scudetto kwa mara ya kwanza tangu enzi ya Diego Maradona, ndiyo kitu anachokilenga kwa mshambuliaji huyo.

"Unapofanya vizuri sana, klabu kubwa kote duniani zinatazama, haswa katika ligi tano bora," alisema Osimhen akiiambia ESPN.

"Kuweza kuvutia klabu hizi za juu kunaonesha kuwa ninafanya vizuri na inanipa motisha ya kufanya mengi zaidi kwa ajili yangu na timu yangu.

"Lakini ninaelekeza nguvu zangu kwa Napoli kwa sasa na wao ndio wenye uamuzi wa mwisho. Nataka tu kuisaidia timu yangu kushinda mechi na kushinda mataji.

"Mwishoni mwa msimu, tutaona kitakachotokea, lakini hilo si juu yangu. Ni kwa klabu ndio itaamua."




# Atsu kuzikwa kiheshima Ghana



**ACCRA,** Ghana

MAKAMU wa Rais wa Ghana, Mahamudu Bawmia, amesema mwanasoka Christian Atsu atapewa mazishi ya heshima kubwa nchini humo.

Mwili wa Atsu, aliyefariki katika tetemeko la ardhi lililotokea nchini Uturuki wiki mbili zilizopita, umerudishwa nchini kwao Ghana.

Ndege iliyobeba mwili wa marehemu ilitua mjini Accra Jumapili jioni na jeneza lake lilibebwa na wanajeshi wa Ghana.

Akizungumza katika uwanja wa ndege wa Kotoka katika mji mkuu wa Accra, Makamu wa Rais wa Ghana Bawmia alisema: "Tulikuwa na matumaini dhidi ya matumaini, kila siku iliyopita, tulisali na kuomba, lakini alipopatikana akiwa amefariki.

"Ni mwanasoka aliyependwa sana na atakumbukwa sana. Ni maumivu makali mno kumpoteza." Na kuahidi kuwa Atsu atapewa mazishi ya heshima".

Atsu alikutwa amefariki siku ya Jumamosi chini ya nyumba yake kusini mwa Uturuki.

Alikuwa akiichezea klabu ya Hatayspor.

Hata hivyo, bado siku rasmi ya kuzikwa kwake haijatangazwa.

Winga huyo aliichezea timu ya taifa ya Ghana mara 65 na kuisaidia timu yake kufika fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2015.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 pia aliichezea timu za Ligi Kuu England, Everton na Newcastle, FC Porto na Vitesse.

318,061/-



# USAJILI DIRISHA DOGO WAIPA JEURI IHEFU

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Ihefu, Zuberi Katwila, amesema usajili walioufanya kipindi cha dirisha dogo kwa kiasi kikubwa umewasaidia na kuifanya timu yao kuwa ya kutisha kwa sasa kwenye Ligi Kuu, huku dhamira yao ikiwa ni kutoshuka daraja, ikiwezekana kupata nafasi kucheza kimataifa.

Akizungumzia kikosi chake ambacho kwa sasa kimekuwa kikifanya vema kwenye Ligi Kuu, Katwila amesema anajivunia kikosi chake kwani kimesheheni wachezaji bora ambao wametoka kwenye lengo la awali la kutoshuka daraja na sasa wanaangalia mbele zaidi kwani wanaweza kabisa kuisaka nafasi ya nne ambayo inaweza kuwapa uwakilishi wa michuano ya kimataifa msimu ujao.

"Kikubwa ni uvumilivu na subira, tulifanya mazoezi kwenye kipindi ambacho hatupati matokeo, ila kipindi cha dirisha dogo kimetusaidia sana kwa sababu tumefanya usajili mzuri na kupata wachezaji bora ambao tunajivunia kuwa nao, wanaifanya Ihefu kuogopwa na timu pinzani na hata wanapokuja kukutana na sisi wanajipanga kisawasawa," alisema Katwila ambaye alikuwa anakaimu, lakini kwa sasa ameongezewa John Simkoko ndiye kocha mkuu wa kikosi hicho, akichukua nafasi ya Juma Mwambusi aliyejiengua kwenye kikosi kile alichodai kuwa na matatizo ya kifamilia.

Ihefu ambayo kwenye mechi za mzunguko wa kwanza ilifika wakati ikawa inaburuza mkia na kutabiriwa kuwa inaweza kuwa moja kati ya timu zitakazoshuka daraja, kwa sasa imepaa hadi kwenye nafasi ya tisa ikiwa na pointi 27.

Imekusanya wachezaji kadhaa kwa kusajili na kwa mkopo toka klabu mbalimbali, nao ni Nelson Okwa na Vicent Akpan, wachezaji wa Kinigeria kutoka Simba, Yacouba Songne, Mburkina Faso aliyetoka Yanga na wengine wengi.

.




Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu Kongamano la Sosho na Mimi kwa kushirikiana na Bodi ya Filamu lenye lengo la kutoa elimu kwa wasanii, linalotarajiwa kufanyika Aprili 29, mwaka huu, Dar es Salaam. Katikati ni mwanzilishi wa Sosho na Mimi, Saida Khaifaw na (kushoto) ni Ofisa Habari wa Bodi ya Filamu, Irene Ngao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Yanga: Sasa ni zamu ya KMC*

INATOKA UK 24

matokeo na wamefanyia kazi kila idara ikiwamo safu ya ulinzi, ushambuliaji na ulinzi.

"Mpango mkakati wetu ni kupambana kuyafuta matokeo ili kujiweka katika mazingira mazuri na kuwa kwenye nafasi mzuri katika msimamo na kujiondoa katika nafasi ya chini," alisema Ally. "Kufungwa na Yanga haitakuwa habari, bali sisi kuwafunga Yanga ni habari kubwa, tunaenda kucheza kwa kuwaheshimu kiufundi."

Alisema mchezo wa leo utakuwa wa kimbinu sana huku wachezaji wao wanahitaji kutuliza akili ili kufikia mipango mikakati yao.

Mwakilishi wa wachezaji wa KMC, Awesu Awesu, alisema morali yao iko juu kwa ajili ya mchezo wao wa leo ili kupambana kutafuta matokeo mazuri dhidi ya Yanga.

"Tumejiandaa vizuri na tuko tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya dhidi ya Yanga, itakuwa mechi ya ushindani mkubwa na kazi kubwa kwetu ni kuona timu inapata matokeo mazuri," alisema Awesu.

## Simba yakiri ubora baadhi wachezaji wake kupungua

INATOKA UK 24

Hata hivyo, baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba wamegawanyika kuhusu timu yao ambayo Jumamosi iliyopita ilichapwa mabao 3-0 dhidi ya Raja Casablanca, mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Baadhi wanamlaumu Kocha Mkuu, Robert Oliveira kuwa upangaji wake usio sahihi na mfumo wake mgumu ndiyo uliosababisha kipigo hicho, wengine wakidai kuwa aina ya wachezaji wengi waliopo kwenye kikosi umri wao ni mkubwa, hivyo kutoweza kuendana na falsafa ya kocha, na wapo walioenda mbali zaidi waliodai karibuni nusu nzima ya wachezaji hawana viwango vya kuichezea timu hiyo, hivyo kikosi kinahitajika kisukwe upya msimu ujao.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Aston Villa | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 02. 25/02/23 | 18:00 | Birmingham City vs Luton Town | 2.90 | 3.15 | 2.45 |
| 03. 25/02/23 | 18:00 | Bristol City vs Hull City | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 04. 25/02/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Blackburn Rovers | 2.45 | 3.25 | 2.85 |
| 05. 25/02/23 | 18:00 | Stoke City vs Millwall FC | 2.49 | 3.15 | 2.85 |
| 06. 25/02/23 | 18:00 | West Bromwich Albion vs Middlesbrough FC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 07. 25/02/23 | 18:15 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.85 | 3.10 | 2.55 |
| 08. 25/02/23 | 20:30 | Schalke 04 vs VfB Stuttgart | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 09. 25/02/23 | 21:00 | Maritimo Madeira vs Santa Clara Azores | 2.50 | 3.10 | 2.85 |
| 10. 25/02/23 | 22:45 | US Lecce vs Sassuolo Calcio | 2.41 | 3.20 | 2.95 |
| 11. 25/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.85 | 3.20 | 2.48 |
| 12. 26/02/23 | 16:30 | Tottenham Hotspur vs Chelsea FC | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 13. 26/02/23 | 17:00 | FC Nantes vs Stade Rennes | 3.20 | 3.20 | 2.23 |
| 14. 26/02/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs Strasbourg Alsace | 2.28 | 3.20 | 3.15 |
| 15. 26/02/23 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.37 | 3.40 | 2.85 |
| 16. 26/02/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs GD Chaves | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 26/02/23 | 18:30 | FC Lugano vs FC Basel 1893 | 2.45 | 3.25 | 2.36 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 22/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1141 | Finland W vs Romania W | 1.32 | 4.86 | 7.23 |
| 14:00 | 5614 | Churchill Brothers vs Kenkre FC | 1.47 | 4.16 | 5.62 |
| 15:00 | 4296 | Inter Turku vs HJK Helsinki | 1.45 | 4.09 | 6.01 |
| 15:00 | 5061 | Queens Park vs Hamilton Res. | 1.76 | 4.25 | 3.37 |
| 16:00 | 1988 | China W vs Republic of Ireland W | 2.30 | 3.41 | 2.69 |
| 16:00 | 5323 | KMC vs Young Africans | 7.00 | 3.40 | 1.51 |
| 16:30 | 1670 | Polokwane City vs Cape Town All Stars | 2.13 | 2.81 | 3.64 |
| 16:30 | 2450 | JDR Stars vs Black Leopards | 1.87 | 2.97 | 4.37 |
| 16:30 | 4096 | Venda Football Academy vs Mm Platinum FC | 2.07 | 2.90 | 3.68 |
| 16:30 | 4655 | Pretoria University vs Magesi FC | 1.75 | 3.17 | 4.67 |
| 17:00 | 2580 | Delhi Dynamos FC vs Jamshedpur | 1.72 | 3.67 | 4.08 |
| 17:00 | 3074 | NK Celje vs ASK Bravo | 1.83 | 3.47 | 3.79 |
| 17:00 | 3482 | Holy Ghost vs Township Rollers | 10.40 | 4.78 | 1.26 |
| 17:30 | 4043 | Rostov vs Ural Yekaterinburg | 2.10 | 3.21 | 3.21 |
| 18:00 | 5287 | Cruz Azul U20 vs Atlas U20 | 2.76 | 3.07 | 2.43 |
| 19:00 | 1300 | Hungary W vs Croatia W | 3.42 | 3.37 | 1.96 |
| 19:30 | 1560 | Olimpija Ljubljana vs ND Gorica | 1.45 | 4.03 | 6.20 |
| 20:00 | 2004 | Municipal Turrialba vs Futbol Consultants Moravia | 3.36 | 3.31 | 2.00 |
| 20:00 | 3098 | Wolfsburg U19 vs Werder U19 | 2.34 | 3.52 | 2.58 |
| 20:00 | 5974 | Lokomotiv Moscow vs Spartak Moscow | 3.62 | 3.46 | 1.87 |
| 21:00 | 2017 | Hertha II vs Berliner AK 07 | 2.81 | 3.54 | 2.17 |
| 21:00 | 3011 | SV Lippstadt 08 vs FC Schalke 04 II | 3.06 | 3.48 | 2.06 |
| 21:30 | 2213 | SG 2000 Mulheim vs Karlich-FV Engers 07 | 5.81 | 4.67 | 1.40 |
| 22:00 | 2767 | AD Carmelita vs Municipal Garabito | 1.24 | 5.39 | 9.11 |
| 22:00 | 3174 | Cronenberger SC vs SC St Tonis 11/20 | 3.42 | 3.73 | 1.85 |
| 22:00 | 3379 | AD Atletico Gloriense SE vs Sergipe SE | 5.19 | 3.32 | 1.65 |
| 22:30 | 1123 | RS Berkane vs FAR Rabat | 2.75 | 2.59 | 2.85 |
| 22:30 | 2334 | Raja Casablanca vs Union Touarga | 1.60 | 3.01 | 7.05 |
| 22:30 | 4502 | Holywell Town vs Prestatyn Town | 1.43 | 4.20 | 5.00 |
| 22:45 | 3863 | Kingstonian vs Herne Bay | 2.10 | 3.42 | 3.01 |
| 23:00 | 3602 | RB Leipzig vs Manchester City | 4.08 | 3.60 | 1.79 |
| 23:00 | 4486 | Inter vs Porto | 1.68 | 3.52 | 4.95 |
| 23:00 | 5228 | Accrington vs Bolton | 3.68 | 3.57 | 1.82 |
| 23:00 | 5337 | AD Grecia vs AD Guanacasteca | 1.99 | 3.37 | 3.32 |
| 23:00 | 5671 | UTC Cajamarca vs Academia Cantolao | 1.49 | 3.89 | 5.80 |
| 23:30 | 3865 | Deportivo Guastatoya vs Santa Lucia Cotzumalguapa FC | 1.41 | 3.65 | 6.40 |

ALHAMISI - 23/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 20:45 | 1591 | Nantes vs Juventus | 4.06 | 3.38 | 1.89 |
| 20:45 | 2477 | CFR Cluj vs Lazio | 3.81 | 3.36 | 1.96 |
| 20:45 | 3404 | Midtjylland vs Sporting Lisbon | 4.01 | 3.66 | 1.83 |
| 20:45 | 3538 | Monaco vs Bayer Leverkusen | 2.26 | 3.55 | 2.90 |
| 20:45 | 4579 | PSV Eindhoven vs Sevilla FC | 2.14 | 3.50 | 3.15 |
| 20:45 | 4955 | Anderlecht vs Ludogorets Razgrad | 1.90 | 3.54 | 3.84 |
| 23:00 | 1794 | Lech Poznan vs Bodo Glimt | 2.16 | 3.40 | 3.20 |
| 23:00 | 1844 | Union Berlin vs Ajax | 2.27 | 3.20 | 3.15 |
| 23:00 | 1904 | KAA Gent vs Karabakh | 1.93 | 3.50 | 3.75 |
| 23:00 | 3182 | Manchester Utd vs Barcelona | 2.43 | 3.28 | 2.83 |
| 23:00 | 3649 | Fiorentina vs Sporting Braga | 1.74 | 3.80 | 4.30 |
| 23:00 | 3738 | FC Basel vs Trabzonspor | 2.30 | 3.39 | 2.94 |
| 23:00 | 3892 | Roma vs RB Salzburg | 1.66 | 3.80 | 4.90 |
| 23:00 | 3956 | Rennes vs Shakhtar Donetsk | 1.67 | 3.93 | 4.58 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Nipashe Jumatano Februari 22, 2023



Atsu kuzikwa kiheshima Ghana UKURASA 22

# Yanga: Sasa ni zamu ya KMC

## ●●● Inaivaa leo kwenye mchezo wa Ligi Kuu, ikiahidi pointi tatu ili kuendeleza furaha ya...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Jumapili, Yanga leo inatupa karata nyingine kwenye Ligi Kuu Tanzanjia Bara ikivaa KMC FC.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo watajitupa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Yanga ambao ni vinara wa ligi hiyo wana pointi 59, huku KMC ipo katika nafasi ya 12 ikiwa imecheza mechi 22 na kujikusanyia alama 23.

**Yanga wanahitaji kupata matokeo mazuri na alama tatu ili kuendelea kuweka rekodi yao ya kushinda baada ya kushinda mechi 21 huku ikipoteza moja katika michezo 22 ambayo wamecheza msimu huu.**

Katika mchezo wa leo KMC watakuwa nyumbani na wataendelea kumkosa mchezaji wao, Hans Masoud.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema maandalizi yanaendelea vizuri licha ya kupata muda mfupi wa maandalizi kwani kikubwa ni wachezaji kuwaandaa kisaikolojia.

Alisema walichokifanya ni kuwaandaa wachezaji wao kiakili na kusahau furaha ya matokeo mazuri ya mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe.

"Tuko vizuri kiufundi, kisaikolojia na kimbinu kwa sababu tunahitaji matokeo mazuri katika mchezo wetu wa kutafuta pointi tatu dhidi ya KMC," alisema Kaze.

Aliongeza: "Wachezaji wote wako fiti kasoro wale ambao hatukuwa nao tangu awali kutokana na Morrison na Mshery Abdultwalib ambao ni majeruhi."

Kwa upande wake Kocha Msaidizi wa KMC, Ahmad Ally, alisema wanakwenda kucheza na timu bora na nzuri, hivyo wataingia kwa tahadhari kubwa kwani wanahitaji pointi.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu na bora kwa sababu kila mmoja wao anahitaji

INAENDELEA UK 23




Kenedy Musonda

## Simba yakiri ubora baadhi wachezaji wake kupungua

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imekiri kupungua kwa ubora wa baadhi ya wachezaji wake kutokana na kucheza michuano ya kimataifa na Ligi Kuu kwa muda mrefu bila kupumzika.

Meneja Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kuna baadhi ya wachezaji wa timu hiyo wamefanya kazi kubwa kwa miaka mitano mfululizo kwenye michuano ya kimataifa, Ligi Kuu na michuano mingine, hivyo kama binadamu hawawezi kuwa na uwezo, kiwango au ubora ule ule waliokuwa nao awali.

"Simba ipungua ubora kidogo, lazima tuwe wa kweli. Kwanza kuna nyota wetu ambao ubora wao umepungua kidogo kwa sababu ya kuchoka, wamefanya kazi kubwa kwa miaka mitano, wamecheza sana kwa miaka yote hiyo michuano ya kimataifa, Ligi Kuu na michuano mingine mfululizo, hakuna binadamu ambaye anaweza kukupa asilimia 100 kwa miaka mitano, Mungu hajamuumba binadamu wa hivyo. Na unafahamu mpira kazi ya nguvu na kutumia akili na muda, unapocheza inatakiwa akili yako ifanye kazi kwa haraka sana, ukifanya kazi hiyo kwa miaka hiyo mfululizo lazima utachoka na kiwango kinapungua, ndiyo maana unaona ubora huo umepungua kwa sasa," alisema Ahmed.

Akatoa mfano mchezaji kama Mohamed Hussein 'Tshabalala', ambaye anacheza hatua ya awali ya michuano ya kimataifa, hatua ya kwanza, mechi sita za makundi na robo fainali kwa miaka mitatu, haiwezekani baada ya hapo atakuwa kwenye kiwango kile kile, ni lazima kitapungua kidogo.

Mbali na hilo alisema wapo baadhi ya wachezaji ambao walikuwa bora, lakini wameondoka kwenye klabu hiyo kwa kuuzwa.

"Kingine ambacho unaweza kuona ubora huo umepungua kidogo kwenye timu yetu, wapo watu wameondoka kwenye timu yetu, ama wameuzwa, au viwango vyao vilipungua, wakauzwa.

Mohamed Hussein 'Tshabalala', anacheza hatua ya awali ya michuano ya kimataifa, hatua ya kwanza, mechi sita za makundi na robo fainali kwa miaka mitatu, usitegenee baada ya hapo atakuwa kwenye kiwango kile kile, ni lazima kiwango kitapungua kidogo.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >